# TAIFA Jumapili

A NATION MEDIA GROUP PUBLICATION




## Vigogo wa BBI walenga kuvuruga Mudavadi kwa kuwakiuka

'JAMVI' 11 - 14

## Siaya yatangazwa kama kaunti zembe katika vita dhidi ya corona UK2


Jumapili, Juni 7, 2020 •KSh30 • TSh500 • RFr300 taifaleo.nation.co.ke No. 20611


### Wakenya walitarajia Rais kulegeza masharti lakini matumaini yao yakagonga mwamba


# UHURU APIMIA WAKENYA HEWA

BENSON MATHEKA NA VALENTINE OBARA

MATUMAINI ya Wakenya wengi kurejelea hali ya kawaida ya maisha kuanzia leo, yalizimwa jana wakati Rais Uhuru Kenyatta alipotangaza kuwa bado Kenya haina uwezo wa 'kujihatarisha' kwa mkurupuko zaidi wa virusi vya corona.

Rais alisema alichukua hatua hiyo kwa sababu juhudi za kuboresha hospitali ili zipambane na ugonjwa wa Covid-19 hazijafanikiwa kikamilifu kitaifa. Pia alitaja idadi ya maambukizi inayoendelea kuongezeka, na uwezo mdogo wa kutafuta wanaotangamana

ENDELEA Uk 2




**"Nimeona watu wakisambaza picha za utani eti leo ni siku ya uhuru. Hili si jambo la uhuru bali linahusu maisha. Tunafanya hivi kuhakikisha tunalinda maisha ya wananchi. Sioni haja ujivinjari kisha uelekee kaburini."**

**Rais Uhuru Kenyatta**

**Kufungiwa (k.m kusafiri ndani na nje ya maeneo)**
- Mitaa ya Eastleigh (Nairobi) na Old Town (Mombasa) kufunguliwa kuanzia leo
- Kaunti za Kwale na Kilifi kufunguliwa kuanzia leo
- Kaunti ya Nairobi na viungani, Mombasa na Mandera kuendelea kufungwa kwa siku 30

**Kafyu (saa zabadilika)**
Muda wa kutotoka nje wabadilishwa ili uanze saa tatu usiku hadi saa kumi alfajiri kuanzia leo

**Shule**
Kufunguliwa kwa zamu kuanzia Septemba 1. Ratiba mpya kutolewa Agosti

**Maeneo ya ibada (k.m makanisa na misikiti)**
Yataendelea kufungwa japo baraza la viongozi wa kidini litaundwa ili kutoa mwongozo kuhusu jinsi ya kuyafungua

**Mikutano (k.m baa, tafrija, harusi)**
Marufuku ya siku 30 zaidi dhidi ya mikusanyiko katika baa, karamuni, na mikutano ya kisiasa

## Seneta Cherargei anusurika katika ajali akitoka kikao cha siri

Na TITUS OMINDE

SENETA wa Kaunti ya Nandi, Bw Samson Cherargei alihusika katika ajali ya barabarani mnamo Ijumaa usiku akitoka katika mkutano wa siri wa Naibu Rais William Ruto, aliyekutana na wazee wa jamii ya Wanandi na baadhi ya wandani wake.

Bw Cherargei alithibitisha kwamba hakupata majeraha mabaya katika ajali hiyo.

ENDELEA Uk 2

**SPOTI:** BALE ASEMA HANA MPANGO WA KURUDI LIGI KUU YA UINGEREZA **UK 16**

# Hasira kaunti ikianikwa kwa uzembe

Na WAANDISHI WETU

WAKAZI wa Kaunti ya Siaya wameghadhabishwa baada ya Rais Uhuru Kenyatta kutaja kaunti hiyo kama mfano wa zilizobaki nyuma zaidi katika vita dhidi ya virusi vya corona.

Akitangaza kanuni mpya jana, Rais alitaja Siaya kama mfano wa kaunti ambazo hazina vitanda vya kutosha vya wagonjwa ilhali kila kaunti ilitarajiwa kujitahidi kwa uwezekano wa kuzagaa kwa mkurupuko wa ugonjwa wa Covid-19.

"Haieleweki jinsi hatujaweza kupanua sehemu za kutenga wagonjwa wa Covid-19. Inasikitisha kuwa hakuna mtu aliyejitokeza kutueleza jinsi fedha zinavyotumiwa," akasema mwenyekiti wa vuguvugu la vijana katika kaunti hiyo, Bw Ben Nyamulo.

Kamishna wa Kaunti, Bw Michael ole Tialal, alitangaza kuwa kaunti hiyo ilipokea Sh97 milioni kutoka kwa serikali kuu na Sh50 milioni zikatengwa kutoka kapu la fedha za serikali ya kaunti hiyo kupambana na virusi vya corona.

Lakini kilichoshangaza ni kuwa, katika hotuba yake, Rais Kenyatta alitangaza kuwa kaunti hiyo ina vitanda 10 pekee vilivyotengewa wagonjwa wa Covid-19 ilhali tayari wagonjwa tisa wameshalazwa katika hospitali ya Siaya yenye uwezo wa kupambana na ugonjwa huo.

Katika Kaunti ya Homa Bay, Mwakilishi wa Kaunti, Bi Gladys Wanga alisifu hatua zilizotangazwa na Rais akisema hali itakuwa mbaya zaidi kama watu wataruhusiwa kusafiri kwenda maeneo ya mashambani.

Askofu Joseph Obanyi wa Kanisa Katoliki katika Kaunti ya Kakamega alisema ijapokuwa serikali ina nia njema kwa kuendeleza kafyu na kufunga baadhi ya miji na maeneo, makanisa yangeruhusiwa kufunguliwa.

"Makanisa yana uwezo na yako tayari kutimiza kanuni za serikali kuhusu ugonjwa wa Covid-19 kama yatafunguliwa. Kufunga kila sehemu kutaumiza nchi," akasema.

Katika maeneo ya Pwani, baadhi ya wakazi walilalamika kuwa hakuna haja ya kufungua Kaunti za Kwale na Kilifi ilhali Kaunti ya Mombasa ingali imefungwa.

Kulingana nao, Mombasa ndiyo kitovu cha shughuli za Pwani kwa hivyo ikiendelea kufungwa ukanda mzima utaendelea kuathirika vibaya.

*Ripoti za Benson Amadala, Dickens Wasonga, Valentine Obara na Mohamed Ahmed*

## Matumaini ya kuruhusiwa kusafiri mashambani yapata pigo, maabadi kufunguliwa karibuni

# Funga fungua za Rais Uhuru

KUTOKA Uk 1

na wagonjwa kama sababu za kutolegeza masharti upesi.

Ilifichuka kuwa viongozi wakuu na wataalamu wanaohusika kufanya maamuzi kuhusu mikakati ya kupambana na janga la corona hawakuelewana, kwani kulikuwa na waliotaka shughuli za kawaida zirejelewe huku wengine wakipinga.

"Baadhi yetu, mimi nikiwemo, tulitaka shughuli zifunguliwe hivi sasa. Bado hilo ni tamanio langu. Ninataka tufungue haraka iwezekanavyo ili tuendeleze uchumi," akasema Rais.

Lakini, akasema, kwa kuzingatia hatari inayokodolea macho taifa hili endapo shughuli za kawaida zintarejelewa wakati huu, iliamuliwa masharti machache pekee yaondolewe na mengine yaendelee kudumu.

"Ni mjinga ambaye hasikilizi wataalamu wake. Wataalamu wetu wametambua kufungua nchi ni kuhatarisha maisha ya Wakenya. Tukifungua tukifikiria kuwa tunasaidia uchumi, mwishowe tutakuwa tumeharibu uchumi huo huo," akaeleza.

Jana idadi ya maambukizi ya virusi vya corona ilipanda hadi 2,600 baada ya watu 126 kupatikana kuambukizwa. Wagonjwa wengine wanne walifariki, na kufikisha idadi kuwa 83.

Rais Kenyatta aliagiza Wizara ya Elimu na ile ya Afya kuweka mikakati ya kuanza kufungua shule kuanzia Septemba. Inatarajiwa shule zitafunguliwa kwa zamu, nayo ratiba ya masomo itatolewa Agosti.

Ijapokuwa makanisa yataendelea kufungwa, kuna matumaini kwani Rais aliagiza Wizara ya Usalama na ile ya Afya kuunda baraza la viongozi wa dini katika muda wa siku saba, ili litoe mwongozo kuhusu jinsi ambavyo ibada zitaendelezwa huku vita vya corona vikiendelea.

Marufuku ya kutotoka nje usiku itaendelea kwa siku 30 zaidi. Hata hivyo, kuanzia leo, kafyu itakuwa kati ya saa tatu usiku hadi saa kumi alfajiri badala ya saa moja usiku hadi saa kumi na moja alfajiri iliyvokuwa.

Rais Kenyatta alisema hii itawezesha wananchi kuendelea na kazi zao bila wasiwasi wa kuvunja sheria.

Jijini Nairobi, kumekuwa na misongamano ya magari baada ya saa moja usiku kwa wiki kadhaa sasa.

Rais pia aliongeza muda wa kutoingia na kutoka Nairobi, Mombasa na Mandera kwa siku 30, akazima matumaini ya wengi walionuia kusafiri maeneo ya mashambani. Kaunti za Kwale na Kilifi zilipata afueni kwani watu wataruhusiwa kuingia na kuondoka kuanzia leo, sawa na mitaa ya Eastleigh (Nairobi) na Old Town (Mombasa).

"Kilifi na Kwale maambukizi yameanza kupungua kwa hivyo tunaanza kufungua. Hapa Nairobi ugonjwa unaenda juu ndiposa tunasema Nairobi si kama Kwale na Kilifi. Tumefungua kule ambapo ugonjwa umeanza kuteremka na tumeendelea kufunga pale ambapo ugonjwa unaenda juu. Hatutaki kueneza ugonjwa kwa kaunti nyingine," akasema.

Mkutano utakaojumuisha magavana wote na viongozi wa serikali kuu utafanywa Jumatano ili kila kaunti itoe hakikisho kuwa itaweka mikakati ya kutosha dhidi ya virusi vya corona.

Rais aliongeza marufuku ya mikutano ya hadhara ya aina yoyote ikiwemo sehemu za burudani kwa siku 30. Hii inaamanisha Wakenya hawatakuwa na uhuru wa kuhudhuria mazishi na harusi katika muda wa siku 30 zaidi.

Safari za kuingia na kutoka nchini pia zingali zimepigwa marufuku kwa muda usiojulikana.



**Afisa wa usalama kutoka katika shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa (NYS) amdadisi mkazi wa mtaa wa Eastleigh, Nairobi jana. Marufuku ya kuingia na kutoka mtaani humo pamoja na mtaa wa Mji wa Kale (Old Town), Mombasa ilikamilika leo alfajiri. Mitaa hiyo imekuwa chini ya marufuku hiyo kwa takribani siku 30.** *Picha/Dennis Onsongo*

Ili kutolea maoni habari hii, nenda kwa taifaleo.nation.co.ke

# Wafugaji walioshtaki Moi hatarini kupoteza mamilioni

Na JOSEPH WANGUI

WAFUGAJI kutoka jamii ya Wasamburu wako hatarini kupoteza mifugo yao kwa kushindwa kulipa deni la Sh8 milioni wanazodaiwa na mawakili wa Rais Mstaafu Hayati Daniel arap Moi.

Hii ni baada ya korti ya kutatua Mizozo ya Mazingira na Ardhi kutupilia mbali ombi la wafugaji hao 249 la kuzuia mnada wa mifugo uliopangiwa kufanywa na madalali wa Naisok Auctioneers.

Jaji Mary Oundo alitupilia mbali ombi hilo kwa kuwa mwakilishi wao, Bw Richard Leiyagu, alibadilisha mawakili wao bila kufuata taratibu na masharti ya mahakama.

Deni hilo linatokana na kesi ambayo walikuwa wamemshtaki Mzee Moi kwa kulipa Shirika la Kuhifadhi Wanyamapori (KWS) ekari 17,105 za shamba linalojulikana kama Kabarak Farm. Shamaba hilo liko eneo la Laikipia Kaskazini, na baadaye lilipewa shirika lingine linalojulikana kama Africa Wildlife Forum (AWF).

Wafugaji waliokuwa wakiishi katika shamba hilo walishindwa kuthibitisha madai yao ya kwamba ardhi hiyo ilikuwa ya babu zao na kwamba walipaswa kuhusishwa katika uuzaji.

Waliposhindwa kwenye kesi, mahakama iliwaamuru kulipa mawakili waliohusika katika kesi hiyo iliyoendeshwa kwa muda wa miaka minane.

"Ni sharti kwamba kwa mabadiliko yoyote ya Mawakili baada ya uamuzi wa kesi, pawepo idhini ya korti na taarifa kwa pande zote za kesi. Pia pawepo idhini kati ya wakili anayemaliza muda wake na anayependekezwa," Jaji Oundo alisema.

Alipokuwa akitoa uamuzi wake katika ombi la kuzuia mnada wa mifugo, hakimu alisema kosa la kutofuata taratibu lililofanywa na Bw Leiyagu na wakili wake mpya haliwezi kuchukuliwa kwa mzaha.

Katika ombi hilo, Bw Leiyagu alisema kuwa Naisok Auctioneers kupitia barua ya tangazo na Kiambatisho, wanataka kuteka ng'ombe 1,300 pamoja na vyombo vya nyumbani na gari lake.

# Jopo la BBI laelekea Mombasa kumalizia ripoti



**Balozi wa Miundomsingi wa Afrika (AU) Raila Odinga katika hafla ya awali.** *Picha/Maktaba*

Na WALTER MENYA

JOPO la Mpango wa Maridhiano (BBI) litaelekea jijini Mombasa kwa kikao maalum kuanzia kesho, kwenye harakati za mwisho mwisho za kuandaa ripoti yake.

Muda wa jopo hilo unatarajiwa kumalizika rasmi hapo Juni 30.

Na linapojitayarisha kwa hatua za mwisho, imeibuka kuwa masuala makuu yaliyogusiwa pakubwa ni ujumuishaji wa jamii zaidi kwenye mfumo wa utawala wa nchi, vita dhidi ya ufisadi, umoja, ustawi wa nchi na ugatuzi.

Jopo hilo limekuwa likifanya kazi katika makundi mbalimbali, ili kuangazia mapendekezo ya kikatiba na kisheria yaliyowasilishwa kwake na Wakenya.

Duru zilizoambia *Taifa Jumapili* kwamba shughuli kuu kwenye kikao hicho itakuwa ni uandishi na tathmini wa kina kuhusu.

"Tumepiga hatua kubwa. Tutakuwa tumemaliza kila kitu katika muda wa wiki mbili zijazo," zikaeleza duru.

Kikao hicho kitafanyika katika eneo la siri, ili kuepuka usumbufu wowote.

Kikao kitawaleta wanachama wote wa Kamati Kuu na wataalamu 30 walioteuliwa, baada ya uzinduzi wa ripoti hiyo mnamo Novemba katika Ukumbi wa Bomas mnamo Novemba.

Wataalamu hao watalisaidia jopo kushughulikia na kulainisha mapendekezo makuu kwenye ripoti. Baada ya kikao hicho, jopo hilo litatathmini upya ripoti hiyo, ambapo baadaye litaikabidhi kwa Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa ODM, Bw Raila Odinga.

Kamati Kuu inaongozwa na Seneta Yusuf Haji wa Garissa kama mwenyekiti. Makatibu wake ni Bw Martin Kimani na wakili Paul Mwangi. Wataalamu hao waliteuliwa kufuatia pendekezo la kamati kuhusu hitaji la kujumuishwa kwao, ili kuisaidia kuiboresha ripoti na kuimaliza katika muda iliyopewa.

# Serikali kuzidi kusaidia wahanga wa mafuriko

Na GEORGE ODIWUOR

SERIKALI itasaidia familia zilizoathiriwa na mafuriko hadi hali ya kawaida itakaporejea, Waziri wa Ugatuzi, Bw Eugene Wamalwa amesema.

Bw Wamalwa alisema mvua inatarajiwa kuendelea kunyesha kwa wiki kadhaa kabla hali ya hewa kubadilika, ndipo iwe salama kwa familia zilizohama makwao kurudi nyumbani.

"Sehemu za maeneo ya Magharibi ya Kenya kama vile Kaunti ya Bungoma bado kuna mafuriko. Hali sawa na hii iko katika maeneo ya Nyando na Karachuonyo katika Kaunti za Kisumu na Homa Bay mtawalia. Tutaendelea kusaidia waathiriwa hadi watakaporudi nyumbani," akasema akiwa mjini Kendu Bay, Kaunti ya Homa Bay jana.

Alikuwa ameandamana na viongozi mbalimbali akiwemo Mwenyekiti wa Baraza la Magavana, Bw Wycliffe Oparanya ambaye alisema magavana kutoka kaunti ambazo zimeathirika na mafuriko waliandika mapendekezo kwa serikali kuu itafute suluhisho la kudumu kuhusu mafuriko.

**20684**

**Ukitaka kuwasiliana na 'Taifa Leo' tuma sms kwa nambari hii ukianza na neno Taifa.**

Alikuwa na Naibu Rais katika mkutano na wazee wa Nandi

# Seneta apata ajali akitoka mkutano wa siri

KUTOKA UK 1

Polisi walisema alitibiwa na kuruhusiwa kutoka katika hospitali moja mjini Eldoret.

"Niko salama salmini. Mungu awabariki nyote," akaandika katika mtandao wa kijamii wa Twitter.

Ajali hiyo ilitokea katika kituo cha biashara cha Kapseret kilicho kwenye barabara kuu ya Eldoret-Kapasabet.

Bw Cherargei alikuwa amekimbizwa katika Hospitali ya St Lukes kwa matibabu baada ya ajali ya hiyo.

Seneta huyo alipata majeraha madogo wakati wa ajali hiyo ya saa nne usiku wa kuamkia jana.

Duru zilisema kuwa Bw Cherargei alikuwa akielekea mjini Eldoret kutoka Nandi ambapo alikuwa amehudhuria mkutano wa faragha kati ya Dkt Ruto na wazee kutoka katika jamii ya Wanandi.

Akithibitisha tukio hilo, Kamanda wa polisi wa kaunti ndogo ya Kapseret, Francis Warui alisema seneta huyo alihusika katika ajali hiyo wakati akielekea Eldoret.



"Ni kweli kwamba seneta alihusika katika ajali katika eneo la Kapseret, lakini tunavyozungumza sasa ameondolewa hospitalini baada ya kutibiwa," alisema Bw Warui.

Chanzo cha ajali hiyo hakikujulikana mara moja lakini polisi walisema huenda gari lake ambapo alikuwa akijiendesha mwenyewe liligonga matuta kabla ya kupoteza udhibiti na kubingiria barabarani.

Bw Warui aliongeza kuwa Seneta huyo wa Chama cha Jubilee, ambaye ni mmoja wa wandani wakubwa wa Naibu Rais yuko katika hali nzuri na hakuna sababu ya kutia umma hofu kuhusu ajali yake.

"Seneta yuko katika hali nzuri na hakuna haja ya kusababisha hofu nyingi kuhusu ajali hiyo. Tunamshukuru Mungu kwamba alitibiwa na tayari ashatoka hospitalini," aliongeza Bw Warui.

Dkt Ruto alifanya mkutano kuanzia alfajiri ya saa kumi na moja Ijumaa na wazee wa Nandi ambao huwa na ushawishi mkubwa kuhusu siasa za Rift Valley.

Ilifichuka kwamba mkutano huo ulikuwa mojawapo ya nyingine nyingi ambazo amekuwa akiandaa nyumbani kwake Sugoi, Kaunti ya Uasin Gishu na Karen, Nairobi kwa wiki kadhaa sasa.

Dkt Ruto anakabiliwa na mawimbi makali ya kisiasa katika Chama cha Jubilee, na inashukiwa uhusiano kati yake na Rais Uhuru Kenyatta umezidi kudorora kwani wandani wake wanaendelea kuadhibiwa katika Seneti na Bunge la Taifa.

Duru zilisema amekuwa akifanya mikutano na viongozi wenye ushawishi kisiasa katika jamii mbalimbali, na vile vile wataalamu wa masuala ya uongozi na siasa ili kujinoa makali kwa maandalizi ya kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu ujao.



**Gari la Seneta wa Nandi Samson Cherargei** *(picha ndogo)* **ambaye alihusika katika ajali mnamo Ijumaa usiku katika barabara ya Eldoret-Kapsabet kwenye kituo cha biashara cha Kapseret.** *Picha/Titus Ominde*



## Bi Taifa

**IDDA NYAWIRA,** 22 ndiye mgeni wetu leo. Binti huyu ni mkazi wa eneo la Baricho, Kirinyaga. Anafanya kazi ya kusambaza bidhaa, marembesho na uanamitindo. Anapenda kutalii maeneo mbalimbali.

*Picha/Joseph Kanyi*

## MUULIZE MJUAJI KOMBO

Kombo, baada ya lockdown tutafanya nini ili tuamshe uchumi?

Frank, Ngong



Set alarm kwa sauti ya juu. Sauti itaamsha kila kitu

SMS SWALI KWA NAMBARI YA SIMU 21603 UKIANZA NA NENO KOMBO

NAIROBI

## Aliyenaswa kwa mauaji ahusishwa na kisa kingine cha unyama jijini

**MWANAMUME** aliyekamatwa kwa mauaji ya mwanamke mtaani Umoja ambaye vipande vya mwili wake vilipatikana katika uwanja wa shule eneo hilo, anahusishwa na mauaji ya mwanamke mwingine ambaye vipande vya mwili wake vilipatikana maeneo tofauti jijini Nairobi Aprili mwaka jana. David Migwi Kariuki, 42, alikamatwa Jumatano na wapelelezi wa Idara ya Uchunguzi wa Jinai (DCI) akiwa mafichoni eneo la Ruai alikohamia baada ya kisa hicho.

Makachero wa DCI waligundua kuwa mwili wa mwanamke ambaye hakutambuliwa uliopatikana katika shule ya msingi ya Tumaini mtaani Umoja ulikuwa umetolewa nyumbani kwa Kariuki iliyoko Amani Court.

Landilodi wake, Bi Nancy Wanja Njuguna aliajiri wanaume wawili kutoa mifuko na tangi la rangi la buluu bila kujua ilikuwa imewekwa vipande vya mwili wa binadamu.

Baada ya vipande hivyo kupatikana, Bi Njuguna, mzoaji taka na mmoja wa wanaume aliokuwa ameajiri pia walikamatwa.

Walipohojiwa, ilibainika kuwa ni Kariuki aliyenaswa kwenye kamera za usalama akiondoka klabu kimoja katikati ya Nairobi akiwa na mwanamke ambaye alipatikana ameuawa na mwili wake kutupwa karibu na Nacico Plaza kwenye barabara ya Landhies mwaka uliopita.

*Na Joseph Ndunda*

NYERI

## Kaunti yang'oa bango la vyoo vya shule lililoibua hasira kwingi

**SERIKALI** ya Kaunti ya Nyeri imeng'oa bango lililokuwa likitangaza ujenzi wa vyoo vya shimo katika shule ya umma, likiwa na picha ya Gavana Mutahi Kahiga.

Bango hilo lililoaminika kuwa la bei ghali liliibua hasira kutoka kwa baadhi ya wananchi na viongozi ambao walimkashifu gavana huyo kwa kupenda kujionyesha kwa miradi midogo.

Mapema mwaka huu, Bw Kagiha alikashifiwa alipobandika picha zake katika chupa za vieuzi ambazo zilisemekana kufadhiliwa na Serikali Kuu.

Mmoja wa waliokashifu bango la ujenzi wa choo katika shule hiyo ya chekechea ni Naibu Gavana Caroline Karungu.

*Taifa Leo* ilipotembelea shule hiyo ya Kahara mnamo Ijumaa, ilibainika bango hilo ambalo pia lilikuwa na picha ya Diwani wa Konyu, Bw Eric Mwangi Wamumbi liling'olewa Alhamisi usiku.

Mlinzi katika shule hiyo aliambia waandishi wa habari kwamba aliagizwa kufunga lango na asiruhusu mtu yeyote kuingia.

*Nicholas Komu Na Stephen Munyiri*

Nation Media Group "Digital Copy"

NAIROBI

## Mtu aliyefungwa kimakosa kulipwa Sh5 milioni

**MAHAKAMA** Kuu imeagiza mwanamume aliyekamatwa bila taratibu zifaazo kuzingatiwa na kungoja miezi 23 kabla kesi yake kusimamishwa alipwe Sh5 milioni.

Bw Anthony Murimi, 28, ambaye ni baba ya mtoto mmoja, alikamatwa kwa madai ya kushiriki wizi wa kimabavu.

Hata hivyo, kesi yake ilikuwa ikiahirishwa kila mara kwa miaka miwili. Ni kutokana na hilo ambapo hakimu alikataa kesi hiyo kuahirishwa tena.

Alimwachilia mnamo Juni 27, 2017 chini ya Kipengele 87 (a) kuhusu sheria za uhalifu.

Baadaye Bw Murimi alimshtaki Inspekta Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Umma (DPP) na Koplo J Ochieng' ambaye ndiye alikuwa mchunguzi mkuu kwenye kesi yake.

*Na Sam Kiplagat*

MALINDI

## Wauzaji wahofia maradhi kutokana na maji taka sokoni

**WAFANYABIASHARA** katika soko la Kwa Jiwa mjini Malindi, Kaunti ya Kilifi, wanalalamikia uvundo unaotokana na maji taka yaliyozagaa sokoni humo hasa mvua inapoendelea kunyesha.

Wakiongozwa na Bw Patrick Karanja, walisema hali hiyo imetokana na ukosefu wa mabomba ya kupisha maji taka na wanahofia kupatwa na maradhi.

"Imekuwa vigumu sisi kuendeleza biashara zetu kawaida hapa kutokana na harufu mbaya ya maji taka. Tumekuwa tukiomba serikali ya kaunti kuweka mabomba ya kupitisha maji taka lakini hilo halijafanyika hadi sasa," alisema Bw Karanja.

Waliongeza kuwa hali ya usafi sokoni humo pia haijazingatiwa kikamilifu licha ya serikali ya kaunti hiyo kuahidi kuajiri vijana watakaotekeleza jukumu hilo.

*Na Alex Amani*

KISII

## Mbunge aomba migogoro ikome chamani Ford-K

MBUNGE wa Kitutu Chache Kusini, Bw Richard Onyonka amewaomba wabunge na wadau wengine wa Chama cha Ford Kenya kuyatatua matatizo yanayokikumba chama binafsi.

Mbunge huyo aliye mwanachama wa Ford Kenya alionya kuwa migogoro chamani inatishia kukivunja.

Alikuwa akiongea jana mjini Nyangusu kwenye hafla ya mazishi ya mfanyabiashara maarufu katika Kaunti ya Kisii.

Chama hicho kimegawanyika kufuatia mpango wa kumbandua Kiongozi wa Chama, Bw Moses Wetang'ula uongozini.

*Na Wycliffe Nyaberi*

Asema ushirikiano wake na Badi utaboresha huduma za jiji kuu

# Rais amtaka Sonko ashirikiane na NMS

NAIROBI

Na VALENTINE OBARA

RAIS Uhuru Kenyatta amemtaka Gavana wa Nairobi Mike Sonko ashirikiane na Idara ya Kuhudumia Nairobi (NMS) kuendeleza mbele jiji hilo kuu.

Akizungumza Ijumaa wakati wa kuadhimisha Siku ya Mazingira Ulimwenguni, Rais Kenyatta alisema ushirikiano wa Bw Sonko na idara hiyo inayosimamiwa na Meja Jenerali Mohammed Badi utasaidia kuleta mafanikio ya haraka kwa mikakati inayoendelezwa kuboresha kaunti hiyo na viunga vyake.

Wito huo ulitolewa wakati ambapo NMS inaendelea kuonekana ikishikilia shughuli tele za kuendesha jiji, huku makao makuu ya kaunti yakibaki mahame.

Katika makubaliano ya Bw Sonko na Ikulu, Kaunti ya Nairobi ilisalimisha idara za Afya, Uchukuzi, Mipango ya Jiji na Ujenzi.

Jukumu lingine lilitajwa kama "shughuli nyinginezo za kufanikisha utendakazi" ambalo wadadisi wanaamini ndilo lilisababisha pia jukumu muhimu la kukusanya kodi za kaunti (idara ya fedha) na usafishaji wa jiji ambao uko chini ya idara ya mazingira, zitwaliwe na serikali kuu.

Wiki iliyopita, Rais Kenyatta alitoa amri ambayo iliifanya NMS kuwa chini ya Afisi ya Rais na hivyo basi kuweka utekelezaji wa mipango yote ya NMS chini yake.

Katika amri hiyo, ilibainika kwamba miongoni mwa majukumu makubwa ambayo NMS itatarajiwa kufanikisha ni ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa umma, uboreshaji makao katika mitaa ya mabanda na uboreshaji wa uchukuzi jijini.

Mnamo Ijumaa, Mamlaka ya Kusimamia Mazingira Kitaifa (NEMA) ilichapisha kwenye gazeti rasmi la serikali mpango wa ujenzi wa nyumba 1,562 katika mtaa wa Pangani, Nairobi.

Wakati huo huo, NMS inaendeleza ukarabati wa barabara za katikati ya jiji ikiwemo kubadilisha maeneo kadhaa ya uegeshaji magari yawe yakitumiwa na waendeshaji baiskeli na wapitanjia.

Ijapokuwa awali Sonko alilalamika sana kwamba alipotia sahihi kwenye makubaliano ya kuikabidhi serikali kuu baadhi ya majukumu, hakujua ilimaanisha NMS ingetwaa majukumu mengi, ameonekana kulegeza msimamo katika siku chache zilizopita.

Wiki iliyopita, alipitisha bajeti ya ziada ya kaunti ambapo, hatimaye, serikali ya kaunti ilikabidhi NMS Sh3.5 bilioni kwa jumla.

Hata hivyo aliendelea kusisitiza ni sharti sheria zifuatwe kikamilifu katika utekelezaji wa maelewano kati yake na Serikali Kuu kuhusu ugavi wa mamlaka ya kaunti.

"Nimeamua kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya wakazi wa Nairobi badala ya siasa duni ambazo zimekumba Nairobi kwa miezi mitatu iliyopita. Kuanzia sasa ninatoa wito kwa kila mmoja wetu tuweke siasa kando, na tutilie maanani hitaji la kuhudumia Nairobi," akasema.



RAIS Uhuru Kenyatta akizungumza Ijumaa wakati wa kuadhimisha Siku ya Mazingira Ulimwenguni. Rais Kenyatta alisema ushirikiano wa Bw Sonko na idara ya NMS inayosimamiwa na Meja Jenerali Mohammed Badi utasaidia kuleta mafanikio ya haraka. *Picha/PSCU*

NYERI

## Pesa zenu zitakuwa salama, Waziri Munya ahakikishia wakulima

WAZIRI wa Kilimo, Bw Peter Munya, amewahakikishia wakulima kwamba fedha zao zitakuwa salama watakapowasilisha mazao yao kwa Shirika la Kitaifa la Wakuzaji (KPCU).

Waziri alisema kuwa serikali imefaulu kuyaondoa makundi yote ambayo yalikuwa yakipora shirika hilo hapo awali, hadi kikafilisika.

Bw Munya alikuwa akiwahutubia wawakilishi wa vyama vya ushirika vya kahawa katika Kaunti ya Nyeri, kuhusu juhudi za serikali kuhakikisha kuwa Sh3 bilioni zilizotolewa kwenye Hazina Maalum ya Kahawa zimewafikia bila matatizo yoyote.

"KPCU sasa imo chini ya udhibiti wa Serikali ya Kitaifa. Kwa hivyo, nataka kuwahakikishia kwamba hakuna fedha zozote za wakulima zitakazopotea," akasema. Aliongeza kuwa chama hicho kiko chini ya usimamizi mpya na kitatekeleza jukumu muhimu kwenye utoaji wa fedha hizo baada ya mikakati yote ya utoaji wake kukamilishwa.

*Na Irene Mugo*

TAITA TAVETA

## Mzozo kusimamia Mtito Andei wazidi

MGOGORO umezidi kati ya Kaunti ya Taita Taveta na Makueni kuhusu ukusanyaji ushuru katika mji wa Mtito Andei.

Jana, maafisa wa kaunti ya Taita Taveta waling'oa bango lililowekwa na madiwani wa kaunti ya Makueni magharibi ya mto Tsavo kuweka alama kwenye mpaka.

Waziri wa Ardhi Mwandawiro Mghanga aliyeongoza shughuli hiyo aliaumu Kaunti ya Makueni kwa kuchukulia suala hilo la mpaka kama mzaha.

Mzozo wa mpaka huo ulianza kutokota tangu 1992 mipaka ilipofanyiwa marekebisho. Uliongezeka mfumo wa ugatuzi ulipoanza kutumika baada ya kaunti ya Makueni kuanza kukusanya ushuru kutoka hoteli na mikahawa iliyoko Mbuga ya Kitaifa ya Tsavo Magharibi.

*Pius Maundu na Lucy Mkanyika*

MOMBASA

## Orodha ya mashujaa wa corona yamsikitisha Joho

GAVANA wa Mombasa, Bw Hassan Joho amesikitishwa na jinsi hakuna yeyote katika kikosi chake cha kupambana na janga la corona aliyetuzwa na Rais Uhuru Kenyatta.

Akizungumza Alhamisi jioni alipopokea misaada zaidi kutoka kwa wahisani, Gavana Joho alidokeza ataweka mpango wa kutuza wale waliojitolea kusaidia Mombasa, hasa mfanyabiashara Abdul Samji ambaye ndiye mwenyekiti wa kamati inayosimamia masuala ya kutoa misaada Mombasa wakati huu wa janga la corona.

"Nilihuzunika hivi majuzi Rais alipotangaza tuzo kwa watu wengi. Hatukutuma jina lake lakini anastahili, itabidi tumtafutie kitu."

*Na Valentine Obara*

POKOT MAGHARIBI

## Naibu Chifu aliyetoweka katika kituo cha afya akishukiwa kuwa na corona apatikana Uganda

NAIBU wa Chifu kutoka Kaunti ya Pokot Magharibi ambaye alitoweka kutoka kituo cha afya akishukiwa kuwa na virusi vya corona, jana alipatikana na kurejeshwa nchini na maafisa kutoka nchi jirani ya Uganda.

Naibu huyo wa chifu wa Kata ya Natemer, Tarafa ya Kiwawa, eneobunge la Kacheliba alitoweka wiki mbili zilizopita.

Jana alirejeshwa nchini na maafisa wa Uganda hadi eneo la mpaka la Alakas ambapo alichukuliwa na maafisa wa usalama wa Kenya. Ilisemekana alipatikana katika mji wa Amudat nchini Uganda akinunua bidhaa dukani.

Alipelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kapenguria na kuwekwa kwenye chumba cha kijitenga.

Kwenye mkao wa wanahabari hospitalini humo, Gavana wa kaunti hiyo Prof John Lonyangapuo alisema kuwa chembechembe za chifu huyo zilichukuliwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufaa na Mafunzo ya Moi, Eldoret kupimwa ikiwa kweli ana ugonjwa wa Covid-19.

Alisema kuwa ukweli utabainika baada ya chifu huyo kupimwa mara mbili kwa kipindi akataka wakazi wakome kueneza uvumi.

*Na Oscar Kakai*

Ukiwa na suala lolote ungetaka kuwasilisha kwetu, tuma sms bila malipo kwa 20684 ukianza na neno 'Taifa'

## Usiende kupiga watu na kusema ninapigania mbingu, maana ya pigania ni fanya bidii ya kupata kitu

# Upiganie mbingu, hii ndiyo siri ya watakatifu



**MAHUBIRI**
Padre Faustin Kamugisha

**"Lakini tukiisha kuteswa kwanza na kutendwa jeuri, kama mjuavyo, twathubutu katika Mungu..."**

**(1 Wathesalonike 2:2)**

Baada ya maneno hayo, akainuliwa, mbele ya macho yao, na wingu likampokea wasimwone tena" (Matendo ya Mitume 1:9).

"Hakuna mtakatifu anayeshinda na kupata taji bila ya kulishindania?" (Mt Jeronimo, padre na Mwalimu wa Kanisa).

Kwa msingi huu, tuombe neema ya kupigania mbingu. Mbinguni ni "ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote" (Efe 1: 20-21).

Kuna hadithi juu ya kijana aliyesema, "Kwangu itakuwa rahisi kuingia mbinguni. Nikiingia mlangoni nitafunga mlango na kufungua, nitauchezesha mlango mpaka Mt Petro akasirike aseme, 'Kama unaingia ingia, kama unatoka toka, hapo ataingia kwa urahisi."

Kuingia mbinguni si rahisi hivyo, lazima kulipigania. Mtume Paulo alipigana, "ninapigana ngumi vivyo hivyo" (1 Kor 9:26).

Usiende kupiga watu na kusema ninapigania mbingu. Maana ya pigania ni fanya bidii ya kupata kitu.

Kwanza, thubutu. Hatuthubutu kwa sababu mambo ni magumu. Mambo ni magumu kwa sababu hatuthubutu. Bwana Yesu ni mshindi aliyekuwa anathubutu. Licha ya upinzani mkali mjini Yerusalemu, Yesu alikaza uso kuelekea Yerusalemu.

Mtume Paulo alithubutu, "Lakini tukiisha kuteswa kwanza na kutendwa jeuri, kama mjuavyo, katika Filipi, twathubutu katika Mungu




kuinena Injili ya Mungu kwenu, kwa kuishindania sana" (1 Wathesalonike 2:2).

Watu wengi wanathubutu mambo ya duniani. Kuna tajiri aliyetoa Sh100 milioni kwa mwanaume atakayeweza kuogelea kwenye kisima chenye mamba na kuvuka bila kushambuliwa na mamba. Wanafamilia wengi walikusanyika. Kabla ya tajiri huyo kumalizia maelezo waliona Bwana mmoja anaogelea akikwepa mamba.

Aliweza kutoka na kupewa pesa Sh100m. Alishangiliwa. Wakiwa nyumbani wanaongea na mke wake, mke wake alimpongeza na kumuuliza, "Uliwezaje, kuogelea?"

Alijibu, "Kuna mtu alinisukuma kwenye maji. Sijui ni nani?"

Mke wake alimjibu, "Ni mimi."

Pili, shuka. Paa chini chini ili upae juu juu. Kupaa kunadokeza kushuka. Yesu alishuka sehemu za hali ya chini: Gethsamane, Kalvari na kaburini.

Neno "alipaa" linadokeza ukweli kuwa alishuka kwanza hapa chini duniani. Kupaa ni kuinuliwa (Yohane 12:32; KKK Na 662). Paa chini chini ili upae juu juu. Panya alimeza dhahabu ya tajiri mmoja. Alimwajiri mwindaji kumuua panya. Wakati akimfuatilia panya, aliona panya wengi wamekusanyika. Mbali na panya hao palikuwepo na panya aliyejitenga na wenzake. Haraka akamshughulikia.

Alikuwa amemeza dhahabu. Alipoulizwa alijuaje?

Alisema, kwa kawaida wenye majivuno wakishapata ujitenga na wenzao. Hawapai chini chini.

Tatu, achia. Yesu alikuwa ni wa kuachia. Msalabani hakukunja ngumi ameachia. Aliachia amani, "amani nawaachieni; amani yangu" (Yohane 14:27). Aliachia. Hamwezi kupeana mikono mmekunja ngumi. Kusamehe ni kuachia.

"Achilieni, nanyi mtaachiliwa" (Luka 6:37). Yesu msalabani hakuwabeba akilini waliomtesa. Aliwasamehe. Achilia uliyembeba. Achilia kumbukumbu mbaya.

Usitwishe akili yako mzigo mzito wa kukumbuka. Niliona picha ya mtu anavuta mkokoteni ambapo kuna kichwa chake. Mzigo mzito unakutwa kichwani. Achia.

Nne, juu chini: Tazama juu, tazama chini. "Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni?" (Mate 1:11). Kuku akinywa maji kidogo anatazama juu kushukuru. Lakini hakai ametazama juu, anatazama chini tena kunywa. Tutazame juu tumshukuru Mungu anayotuepusha na Corona. Tutazame chini, tunawe mikono. Tutazame juu tumuombe Mungu atukinge, tuwe makini namna tunavyopiga chafya.

Tutazame juu tumuombe Mungu atusaidie tuwe na mavuno ya kutosha, lakini tutazame chini tulime mashamba.

Tano, lipa. Lipa deni la upendo. Tunasali, "utusamehe madeni yetu" (Mt 6:12). Dawa ya deni ni kulipa.

Kuna mtoto ambaye aliulizwa darasani na mwalimu, "Baba yako akikopa pesa benki 50,000 na akakopa kwa jirani yake 50,000, atalipa jumla ya shilingi ngapi?"

Mtoto alijibu, "Hatalipa hata shilingi moja." Mwalimu alikasirika na kumuuliza tena.

Mtoto alijibu hivyo hivyo. Mwalimu alitishia kumwadhibu. Mtoto alimwambia mwalimu, "Mwalimu unajua hesabu, humjui baba yangu. Si desturi yake kulipa madeni."

Sita, mwache. Tumwache Yesu aende. Maria Magdalena alipotaka kumgusa Yesu, Yesu alisema, "Usinishike, kwa maana sijapaa bado kwa Baba" (Yohane 20: 17). Ni kama alisema, "uniache niende."

Kupaa ni kutokuwepo-kuwepo. Yesu angeendelea kuwepo kimwili labda angekaa tu Yerusalemu au Galilaya. Katika ulimwengu wa kiroho sasa yupo kila mahali. Ni omnipresent. Ulipo yupo. Yeye alisema, "mimi nipo pamoja nanyi sikuzote hadi ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20)

Angebaki duniani kuona kungechukua nafasi ya kuamini.



## ENGLISH SET ONE APRIL 2020 MARKING SCHEME

## PAPER 2 (Comprehension, Literary Appreciation and Grammar) Time: 2 Hours 30 Minutes

### Section B: (25 marks) Compulsory novel: *Blossoms of the Savannah-H.R Ole Kulet.*

7) With reference to the excerpt, explain the use of any two stylistic devices. ***(4marks)***

- Use of local dialect- presentation of the song in local dialect.
- Use of oral literature genre; song
- Symbolism-tinkling bells representing Taiyo and Resian in the context of the culture.

*(Accept any relevant stylistic device that is well-illustrated)*

8) What happens immediately after this excerpt? ***(2marks)***

Taiyo is stupefied and she recounts how she did well in music during her high school times and how disappointed she was when she remembers how her father denied her a chance to explore her talent.

9) Explain the meaning of the following words as used in the excerpt. ***(4marks)***

(a) Demurel- reserved/characterised by shyness.
(b) Whirling- rapid movement in circular motion.
(c) Broke out- disintegrated from their patterns/ arrangements.
(d) Tinking bell- make a succession of short, ringing sounds, as a small bell.

### Section C: Oral Narrative (20 marks)

Long ago, there was famine in Gikuyu land. This famine had made the cows and goats to die. Only human beings were left and even them, it could be seen that they were not going to live much longer. Now the people asked themselves, "What shall we do?" It was decided that the most beautiful girl, one called Wanjiru should be sacrificed to god so that the rain could fall. She was brought to a place where there was a big river. She started to sing:

Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
My father said I should be lost. I should be lost
My mother said I should be lost. I should be lost
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
She went down on her knee, she sang:
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
My father said I should be lost, I should be lost
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
The water reached the waist, she sang
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
My father said I should be lost, I should be lost
My mother said I should be lost, I should be lost
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
The water reached the neck, she sang
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
My father said I should be lost, I should be lost
My mother said I should be lost, I should be lost
Rain fall and make this ridge green
Make this ridge green
The head went in
Very heavy rains fell on this land. The grass and a lot of food grew and the people began to feel better. Now, where Wanjiru went she found her people who had died before her. These people had a lot of cows and goats. They asked her what she would like. She said she wanted cows and goats. She was given many goats and cows and then she was told to lie down. When she woke up she found that she had returned back to her people. She woke up at a place where there was a river and she had her cows and goats. When the people saw her they rejoiced greatly.
The story ends there.

Adapted from: ***The Oral Literature of the Gikuyu by Wanjiku Kabira and Karega Mutahi.***

Questions

1) Why do you think this community makes the choice of a beautiful girl such as Wanjiru to sacrifice to god so as to receive rain? ***(1mark)***

They give the most beautiful girl so as to appease god.

2) Identify two social/cultural aspects of the society from which the narrative is taken. ***(2marks)***

- Sacrificing to god so as to appease to give rain.
- Singing of songs at different times in life.
- The community offers prayers/supplications more so when faced with eminent danger.
- They commune/communicate/value the spirits/ dead relatives.

3) In point form, list how events follow each other in this story. ***(4marks)***

- A severe famine hits the land and a decision to sacrifice Wanjiru is reached. She is taken to a big river where she sings repeatedly as the water as the water level rises.
- There is a heavy down pour
- She goes to the spirit world where she is rewarded with many cows and goats and asked to lie down.
- She wakes up to find herself at the big river.
- The villagers rejoice greatly.

4) Which functions does this song serve in this narrative? ***(3marks)***

- The song is a supplication/ prayer. In her prayers she says: "Rain fall and make this ridge green. Make this ridge green."
- It serves to show the mental anguish she goes through knowing that she has been picked to be the sacrificial sheep to save the whole community from the debilitating famine. She anguishes: "My father said I should be lost, I should be lost."
- The song helps enhance the sombre mood that engulfs the village.

5) Describe any one character trait of the villagers in this narrative. ***(2marks)***

- The villagers are pious/ religious. They consult from god what they needed to do so as to have rains. They also readily accept to offer the sacrifice prescribed by god.
- They are decisive. They decided to offer Wanjiru as sacrifice to their god.

6) Describe Wanjiru's tone in the song. ***(2marks)***

The tone is resigned. ✓ She is resigned to fate. She feels that there is nothing she can do to overturn her parents' decision to sacrifice her to god. ✓

7) Identify two elements of fantasy in this story. ***(2marks)***

- The river responding to Wanjiru's song and rising until they submerge her completely.
- Wanjiru going to the land of spirits and even talking with them. Returning back to the land of the living.

8) Apart from the use of fantasy and song, identify and explain two features of oralnarration employed in this narrative. ***(2marks)***

- Rhetorical questions- "What shall we do?" this question helps the readers to understand the magnitude of the dilemma the villagers face.
- Opening formula- The story starts with, "Long ago..." signals the start of the story
- Closing formula- The story ends there". This formula signals its end.
- Repetition- My father said I should be lost. I should be lost.
  -My mother said I should be lost. I should be lost.

*(Expect three features with valid illustration)*

9) What does this phrase mean? "My father said I should be lost." ***(1mark)***

It means that her father wanted her dead.

10) Answer the following question according to the instructions given in brackets. ***(1mark)***

Very heavy rains fell on this land. [Change the voice]

- On this land, fell very heavy rains.

### Section D: Grammar (15 Marks)

1) Pick the odd one out from the following list of nouns. ***(3marks)***

a) Valley, Ngugi Wa Thiongo, House, Bottle, Pen, Kernel

- Ngugi Wa Thiongo( Proper Noun)

b) Tree, Desk, Hurry, Car, Boy, Table

- Hurry (Abstract Noun)

c) Sunshine, Ice cream, A bar of chocolate, Passer-by

- A bar of chocolate (Collective Noun)

2) Complete the following sentences using appropriate article. ***(3marks)***

a) There was **__a__** university student playing **_the__** flute.
b) Of all the stars, **_the__** sun is the biggest and **_the__** farthest.

3) Fill in the blank spaces with the correct form of the word in brackets in each of these sentences. ***(2marks)***

a) The wind has **__blown_____** [blow] off the roof.
b) Menju **__has_____** [have] to walk home every now and then.

4) Explain the difference in the meaning of each of the following pairs of sentences. ***(2marks)***

a) Lydia found the empty room.
The room was already empty.
b) Lydia found the room empty.
The room which had items was found empty. (Things had been removed)

5) Use appropriate punctuation marks in the following sentences. ***(3marks)***

a) Name the by-products of petroleum.
•Name the by- products of petroleum (use of hyphen)
b) You must buy a new road license said the traffic officer to a matatu driver.
"You must buy a new road license," said the traffic officer to a matatu driver. (Use of quotation marks)
c) Who does not know that you visited Mandela?
Who doesn't know that you visited Mandela? (Use of apostrophe)

6) Replace the underline words with one word. ***(2marks)***

a) He was accused of stealing knives, forks and spoons- Cutlery
b) The brothers and sisters fought over their parents' property- Siblings

## PAPER 3 (Imaginative Composition And Essays Based On Set Text)

Paper 101/3 is intended to test the candidate's ability to communicate in English. Communication is established in different levels of intelligibility, correctness, accuracy, fluency, pleasantness and originality. It is the linguistic competence shown by the candidate that should carry most of the marks.

*(**NB**: The candidates should begin with the prescribed statement. If not deduct 2 marks – AD Category – marks)*

**A 16 – 20:** The candidate deliberately manipulates language to serve his purpose.

**B 11- 15:** This class is characterised by greater fluency and ease of expression. The candidate demonstrates that he can use English as a normal way of expressing himself.

**C 6 – 10:** The candidate communicates understandably but only more or less clearly. He is not confident with the language.

**D 01-05:** There is generally no communication.

Question 1 a

- Must be a story. If not deduct ***4 marks*** AD
- Must begin with the given sentence. If not deduct ***2marks*** AD

Question 1 b

- It must be a story. If not deduct 4 marks (AD)
- The story must emanate and link up with the saying given. If not, treat as irrelevant and deduct upto ***4 marks*** (AD)
- The saying need not be the title of the story.
- The saying need not begin or end the essay, but the moral should clearly indicate it is implied

Question 2: Play; ***Henry Ibsen, A Doll's House***

"Looks can be deceptive" Drawing illustrations from the play A Doll's House, justify the above assertion.

Introduction

The world is characterized by illusions where what you see is not always what you get. Truly, all that glitters is not gold. Nora's marriage to Torvald seems like a perfect, happy marriage but it turns out to be a suffocating prison for Nora.

Body/Content

Nora seems like a silly, childish woman that is extravagant, hardly self-reliant and only good for housekeeping. However, her actions prove that she is wise, mature and strong willed. Her husband refers to her as a little squirrel and a little spendthrift. Torvald overworks himself and falls dreadfully ill. She borrows a loan of 250 pounds when her husband falls sick in order to facilitate a year long vacation in Italy for him to get some rest as recommended by the doctors. She does needle work and crocheting to pay off the loan herself. She also saves the money she gets from her husband so she's not a spendthrift after all. This is great sacrifice. When her husband rebukes her for borrowing the money, she leaves him. This shows her strong will and independence. It turns out that she was never happy after all. Indeed, things are not always as they seem.

Torvald seems like a loving, strong, benevolent husband. Later it is realize that he is petty, selfish and cowardly. He is a vain man who only cares about his reputation and what others think of him. The reason he gives for wanting to dismiss Krogstad is that he assumes an overly familiar tone

Nation Media Group "Digital Copy"

when others are around. Even his wife finds this narrow-minded. He is too weak to deliver the promise to risk his life's blood and everything for Nora's sake. When he gets wind of Krogstad's impending blackmail, he calls Nora a criminal and a miserable creature and forbids her from raising the children. He is fearful of being exposed.
All that glitters is not gold. At first, Krogstad seems to be a bitter, vengeful extortionist but we later realize that he is actually merciful and sympathetic. Nora borrows a loan of 250 pounds from him and forges her father's signature in the process.
Torvald Helmer plans to dismiss Krogstad from his position at the bank after he is made manager. Krogstad is forced to blackmail Nora in order to keep his job and rebuild his reputation. He writes a letter to Torvald with the details of his secret transactions with Nora. He does all this for his two sons. When he gets reunited with Mrs. Linde his old flame, he recalls the letter revealing his merciful side. Krogstad is an earnest lover. Things are not always as they seem.
Doctor Rank is introduced to us as a very good friend to the Helmer's. Nora says that he is Torvald's best friend. He visits them on a daily basis. Little did we know that he is secretly attracted to his best friend's wife. He even confesses this to her. His true motive for the daily visits is his love for Nora.
Lastly, the Helmer's marriage appears loving but it is not. It is full of lies, pretence, play-acting and an unequal relationship. At first Torvald seems like an affectionate caring husband calling her pet names and giving her money and Nora appears happy, flirting with him and playing with the children. Cracks appear when we come to know of the deception. She lies about trivial things like eating macaroons to serious stuff like borrowing a loan without her husband's knowledge. She says she got the money from her father. Torvald is also seen as a selfish man who does not love Nora but only cares about public reputation. Nora acts childishly but hides her true nature from her husband. Eventually she is forced to leave Torvald. She says that she was not happy at all.
Surely, things are not always as they seem.
**Conclusion**
In brief, do not judge a book by its cover has been validated by the characters appearance or perception is really different from their actions and personalities. Therefore, It is true to say that things are not always as they seem.

- Introduction- ***2marks***
- Body 3:3:3:3- ***12marks***
- Grammar- ***4marks***
- Conclusion- ***2marks***
- Accept relevant credible conclusion

Question 3a: The Short Story; ***Moran (Ed.) ,Memories We Lost and Other Stories.***
With illustrations from Mariatu Kamara.'s 'The President', Justify the assertion of the statement: Political strife cause suffering to the citizens
**Introduction**
In politics, sometimes there may be dissenting factions which may flare up to violence. Whenever that happens, the citizens suffer either physically or mentally.
**Body/content**
To start with, innocent students are subjected to physical and mental suffering. The narrator Mariatu Kamara suffers in the hands of her captors – the rebel soldiers who chop off both her arms. This causes her such excruciating pain that she loses consciousness. Besides, she suffers psychologically when the rebel soldiers celebrated their brutal action and taunted her to go and ask the president to give her new hands. The rebel soldiers did all these because they wanted to overthrow the government whom they accused of corruption.
In addition, the rebel soldiers attacked Marnamo village where they killed as many as a hundred people. They also captured and tied Mariatu Kamara's two cousins Ibrahim and Mohammed. They also dragged her other cousin, Marie's youngest daughter by the hair. Although these three cousins survived death, both their arms were cut off. The ordeal was indeed quite devastating.
Furthermore, the amputees who totalled to more than four hundred resided in a camp. The camp was in a deplorable condition. Besides the amputees, there were four times as many people, most of whom were family members who had moved there to take care of the injured. Yet the camp was the size of a football stadium. The camp was filthy with litter and the smell of rubbish, dirty bodies and cooking food was sickening. Again, the amputees earned their living from begging in the streets, a practice some of them hated.
Moreover, even when the narrator relocates to Toronto where she hoped to fulfil her dream of reading and writing, she suffers setbacks. Once enrolled in school, she was really struggling to write with amputated arms. The teacher had to be patient with her and when taking tests and exams, she had to be given extra time to complete.
**Conclusion**
In conclusion, political leaders should embrace peaceful means of resolving their disputes before it flares up to violence. This will spare innocent citizens the kind of suffering they go through.

- Introduction- ***2marks***
- Body 3:3:3:3- ***2marks***
- Grammar- ***4marks***
- Conclusion- ***2marks***

Question 3b: Drama ***(David Mulwa, Inheritance)***
"Moral decadence is the order of the day in the society." Basing your arguments on 'Inheritance' by David Mulwa, write an essay to validate the veracity of the statement.
**Introduction**
Humanity and social justice should be a norm in any social set up where an individual in that society is accepted and treated equally. That is no longer observed. People have adopted vices and indulge in activities that only benefit themselves regardless of the consequences, hence making their social standing in the society questionable and the responsibilities bestowed upon them are not fulfilled. This is evident in the society presented in the play Inheritance by David Mulwa, where Lacuna messes up the state due to his egocentric nature and greed for power.
**Body/ content**
**Greed and selfishness.**
Leader Lacuna and his cronies use public resources to enrich themselves.
Lacuna is greedy for power and this makes him kill his own father, King Kutula XU in order to become the leader of Kutula.
Lucuna borrows moneys from foreign countries to use it for development of Kutula. However, he embezzles the money by buying an aircraft for personal use.
He carelessly gives money to his cronies and deposits money in foreign accounts in Canada, Swiss, Luxemburg and Manhattan. This causes suffering to the people of Kutula.
Due to his selfishness, Lucuna kills Judah Zen Melo for not to allowing him to Marry his daughter.
**Oppression and exploitation.**
Lucuna Kasoo is an oppressive leader. He poisons his own father King Kutula XV
The people are forced to work without rest and they only rest when they are dead.
The black man is sentenced to work for the white man till death.
The leaders in power forcefully take people's property. Tamina loses her house, land and cars.
Those who raise their voices to criticize the government are in danger of being killed. Judah Zen Melo is beaten up for refusing to kill his brother Bengo who is a critic of the government. Zea Melo cannot easily find a job since nobody is willing to employ him. His land is taken.
Lulu is forcefully locked up at Lucuna's palace. He wants to make her his wife against her wish.
Bango is jailed.
**Corruption.**
Lucuna borrows money meant for development but embezzles it.
The people's sweat is poured in Lucina's porous pockets as he deposits public funds in his foreign banks.
- Bribery- Lucina wants a bribe to kill Bengo whom he considers a thorn in his leadership.

The people are given handouts and this makes them sing praises to Lucina.
They become blind to the truth.
Lucina is nepotic; He favours his own tribesmen, kinsmen and concubines.
**Abuse of office**
Those in power disregard their subjects. They use their power to dismiss Judah Zen Melo for refusing to kill his brother.
Chipande uses his power to purchase Tamina's land at a very cheap prize. He later influences Lucina not to give anyone licence to grow coffee since he does not want competition.
Lucina uses his power to employ his own tribesmen and kinsmen. This is after he is confronted by the employees who protest and rebel against his leadership. He sacks them all and employs his people.
Lucina uses his power to have people killed. He orders the killing of all deserters.
He also uses his power to remove the inhabitants of the valley so that foreigners can occupy it.
Lucina uses his power to arrest and lock up Lulu in his palace. He wants to marry her forcefully.
**Dictatorship / Authoritarian.**
Lucina takes over power forcefully after killing his own father, king Kutula XV
The leaders order the killing of people.
The people are detained arbitrary.
Lucina uses dictatorship to freeze employees' salaries after his foreign accounts are emptied by Robert
He increases the tax profits of companies and business and keeps it for himself.
**Inefficiency**
The government as led by Kutula does not do its work well.
Lucina takes a loan meant to fund the mining of silver. He fails to follow up the money and production of silver. He does not care whether they are making a loss or a profit.
When the production of silver reduces by 15%, Lucina is not aware. He only gives order without monitoring.
Due to his inefficiency, Lacuna, does not keep records of expenditure on the thirty billion loan extended by Planet World Financiers Limited to salvage Kutula's economy.
**Conclusion**
In conclusion, Lacuna's morality being questionable has caused the subjects in Kutula's state to be hopeless in terms of their daily expectations; their lives have been messed up due to the bad leadership depicted by Lacuna.

- Introduction- ***2marks***
- Body 3:3:3:3- ***12marks***
- Grammar- ***4marks***
- Conclusion- ***2marks***

Question 3c: Novel; ***'The Pearl' by John Steinbeck***
"Juana and Kino complement each other in their family. With close reference to the novel, 'The Pearl' validate the truth of the above assertion.
**Introduction**
In any relationship, there are no two people who are exactly the same in terms of personality. Individuals have their strengths and weaknesses. For the relationship to thrive, individuals should use their strengths to complement one another. This is the case with Kino and Juana in the novel 'The Pearl" by John Steinbeck.
**Body/content**
To start with, as Kino moved forward to tackle the scorpion that posed danger to Coyotito, Juana repeated an ancient magic to guard against the evil and muttered a Hail Mary between clenched teeth. After the scorpion bit Coyotito, Kino is preoccupied with beating the scorpion and stomping it until it was only a fragment and a moist place in the dirt. While on the other hand, Juana is busy sucking out as much poison as she can out of Coyotito's wound in an attempt to save his life.
Furthermore, Juana complemented Kino by providing support during his low moments. When Kino suspected that the pearl buyers were cheating him of the real value of the pearl, Juana tugged at his back. When he turned and looked in Juana's eyes, he had renewed strength. When Kino finally makes a decision, to go and sell the pearl at the capital, he sat brooding on his sleeping-mat. Juana watched him with worry, but she knew she could help him best by being silent and by being near.
In addition, Juana becomes a voice of sanity when Kino appeared to be headed for self-destruction. When Kino asserted that he was a man, Juana knew that it meant that Kino would drive his strength against a mountain and plunge his strength against the sea. Juana knew that Kino was headed for self-destruction. She decided to intervene by following him believing that as a woman, she would be the voice of reason, caution and her sense of preservation would cut through Kino's manness and save them all.
Then Juana inspired hope in an otherwise hopeless situation. When Kino realized that the trackers were following them, helplessness and hopelessness swept over Kino and he suggested that he should let the trackers take him. However, Juana instantly offered encouragement to Kino. She tried to convince him that if he gave himself up, chances are the trackers would kill him, his wife and their child. Kino was able to see her point of view and decided to fight on. They proceeded to the mountains where Kino hoped they would lose the trackers.
**Conclusion**
In conclusion, it is evident that Juana's strength of character came in handy whenever Kino's strength wavered. As such their marriage thrived despite the many challenges they encountered.

- Introduction- ***2marks***
- Body 3:3:3:3- ***12marks***
- Grammar- ***4marks***
- Conclusion- ***2marks***

*(**NB**: Accept any relevant introduction and conclusion)*

Nation Media Group "Digital Copy"

# USHAIRI WENU

## Hongera Madaktari

Utumishi ni kipaji, kutoka kwake Muumba,
Hutupa kwa ufaaji, kwa wake aliooumba,
Hakika wauguzaji, shughulini mnatamba,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

Mwaingia hatarini, afya zetu kuzilinda,
Kwa mapenzi nyoyoni, migongo mnaipinda,
Wazalendo naiteni, taifa bora mwaunda,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu

Tangu mjo wa Korona, mmekuwa m mbioni,
Kuwaona wamepona, wote walo atharini,
Vita hivi mwapigana, sante toka moyoni,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

Hongera wapendwa wetu, kofia twawavulia,
Twainua mikono yetu, saluti kuwapigia,
Msione siyo kitu, maisha kiokolea,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

Serikali nawaomba, motisha muwapatie,
Silegeze nayo kamba, vifaa wakabidhie,
Janga hili siwakumba, afyazo wazikingie,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

Nawaomba nyi Wakenya, tufuate mawaidha,
Kawaida kituonya, watuepushia adha,
Maradhi yasije penya, milini kadha wa kadha,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

Karima ninakuomba, uwajaze na hekima,
Sifa zako twaziimba, kwa matendo yao mema,
Daima tutautamba, ufanisi walochuma,
Hongera madaktari, Mola atawakirimu.

*SIMON M. WACHIRA,*
*Shule ya Msingi Mathia,*
*Kirinyaga.*

## Najiunga na Mjengo

Wezanguni ninakiri, sijajenga maishani
Ila sasa nafikiri, la kufanya mtaani
Japo pia ni hatari, kwa afiya ya mwilini
Sina budi kutangaza, kujiunga kwa mjengo

Nimeshindwa la kufanya, sina hela mfukoni
Ufukara wanifinya, nahisi njaa tumboni
Hali 'menisinya, na kuamua akilini
Sina budi kutangaza, kujiunga na mjengo

Usingizi nimelala, na riwaya nimesoma
Mara moja ninakula, sukumawiki kwa sima
Nimeyandika Makala, na shambani nimelima
Sina budi kutangaza, kujiunga na mjengo

Kazi hii ya kujenga, ni sulubu kwa mwalimu
Ninapochota mchanga, na simiti yenye sumu
Ninashindwa kujikinga, dhidi ya hizi dhulumu
Sina budi kutangaza, kujiunga na mjengo

Unajenga siku nzima, asubuhi na jioni
Haupaswi kusimama, na kuketi kivulini
Mwili nzima itauma, ulalapo kitandani
Sina budi kutangaza, kujiunga na mjengo

Ningekuwa darasani, singeenda kwa mjengo
Ningefunza ya bukuni, na kutimiza malengo
Silabasi hapo Juni, ningefungia mlango
Sina budi kutangaza, kujiunga na mjengo.

*MWALIMU GODWIN EMOCHI,*
*Shule ya Upili ya Missions of Hope,*
*Ndovoini.*

## Siasa Mwaweka Mbele

Vilio vimekithiri, wananchi kunyanyaswa,
Metutembelea duri, akili zetu menaswa,
Kila siku ni ghururi, eti habari twapaswa,
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

Magonjwa yametukumba, twamenyana nayo kweli,
Wengine kuchukua kamba, kujiondolea hali,
Viongozi mlopamba, hamuoni mushkeli,
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

Katukondolea macho, zinazokata kuwili,
Kutia kinywani nacho, hakipo tena kamili,
Kimeadimika hicho, njaa zaidi ni kali,
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

Kadhongo kila kuchao, twashuhudieni sisi,
Kwikwi twalia kilio, ukomo zafika kesi,
Tutapatani hakio, tunotazamia sisi?
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

Vya faragha vikao, mwavipanga viongozi,
Mkitazama vioo, na hasira za mkizi,
Kiondoa wengineo, eti ni kuchapa kazi,
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

Tuwe na sera kamili, tuimarishe uchumi,
Janga la korona hili, yatufaa kujihami,
Kwa yakini ni kali, lisofaa siasami,
Siasa meweka mbele, Wakenya wakiteseka.

*JESSE CHEGE M,*
*(Malenga Mzalendo),*
*Chuo kikuu cha Egerton,*
*Bewa la Njoro.*

## Udugu Watokeapi?

Wataka niliza tena, unichokonowe donda,
Lilokesha kunipuna, na puani kunivunda,
Leo wajipa ungwana, ni nduuyo wanipenda,
Nieleza leo hini, udugu watokeapi?

Kipindi naumwa moyo, vilingeni ulicheka,
Ukiwa naye nduuyo, cheche zikiwatoka,
Machweo hadi mawiyo, matusi hamukuchoka,
Nieleza leo hini, udugu watokeapi?

Nilikueleza bure, kuwa hili ni buchari,
Hutumiwa kwa wavyere, wanunuwapo bingiri,
Kwako pia kinyenyere, ukakatiwa kidari,
Nieleza leo hini, udugu watokeapi?

Ndilo lilo hilo jisu, hutumikishwa wateja,
Yeyote halimhusu, hukatia mwenye haja,
Nawe sasa lakubusu, waanza sasa leleja,
Nieleza sasa hini, udugu watokeapi?

Wataka usaidiwe, makali umeyashika,
Umeyahisi mwenyewe, waona damu yatoka,
Wataka uhawiniwe, nami hasa ndo wataka,
Nieleza sasa hini, udugu watokeapi?

Vipi leo wanitaka, enzi hizo kinikana?
Nilokwamba kakufika, wangu wema wauona,
Matusi ulonipaka, hauoni soni bwana!
Nieleza sasa hini, udugu watokeapi?

Ulanda siyo mwandani, hukata pasi kujali,
Ungakuwa wa zamani, mzuri wa kulla hali,
Uendapo benibeni, hukuchanja kwa makali,
Nieleza sasa hini, udugu watokeapi?

*RAMADHAN ABDALLAH SAVONGE,*
*"Malenga Wa Nchi Kavu",*
*Kivumanzi.*

## Samehe Yetu Makosa

Bwana mungu nakuomba, tusikie wako waja,
Mizukozuko yatukumba, nzige korona wakaja,
Adinasi uliumba, kwa mikono wewe soja,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

Hekaluni tulipofika, kasahau yako nyumba,
Biashara kuhusika, na kufanyika ndumba,
Eneo la kukatika, kuliko mziki rumba,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

Tukakana kuabudu, twainamia miungu,
Vya dunia kahusudu, kumshinda wetu mungu,
Husuda nio mdudu, neno tu la kumi fungu,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

Bwenyenye awafilisi, yakhe kwa yote njia,
Wamekuwa ibilisi, watu chini wanalia,
Wajuayo ni irisi, kutojalisi hisia,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

Kumezidi utapeli, tunataka watusifu,
Juzi ilizama meli, tukalaumu machifu,
Miaka kumi ya reli, jasiri anaarifu,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

Nafika leo hatima, maozi yangu mi kwake,
Nisizidi hichi kima, nikaja nipigwe teke,
Simamani nazi wima, korona na atoeke,
Ewe mola maulana, samehe yetu makosa.

*KWOBA BARASA,*
*Bumula.*

## Wewe Hela

La awali nilinene, jina lako mabruki,
Wahdi uso na mwengine, Allah! Huna mshiriki,
Nayasemeza mapene, nistiri ya razaki,
Tuokoe subuhana, jini hili la sarafu.

Ni kitambo tangu kale, makucha liyachomoza,
Kipaa kama mshale, wana wari kuchombeza,
Unatuwasha upele, pesa kweli metuweza,
Tukuite ni hasidi, jina hilo ulitwae.

Si shani sioni soni, dunia kuenda resi,
Unguliko li moyoni, na fikira zangu hasi,
Pesa sasa hwezekani, kukuasa tena basi,
Si heko kwangu huzuni, pesa kutupa wahaka.

Mwanzilishi namsaka, anipe wake wasaa,
Kwa uwazi namtaka, yasirini kusikia,
Asogelee shubaka, matabu kunitolea,
Aliwaza kitu gani, pesa kutugundulia,

Kwa majina huna moja, nani asiekujua,
Ukiacha ya lahaja, na misimu notujia,
Ya mtaani yatungoja, twabaki kukwangalia,
Kitwani yanakoroma, mawazo yaso na tija.

Si mavumba pia mbwasha, pesa, hela, na dinari,
Dirhamu unatukosha, tusisahau dolari,
Kwa visawe hutoisha, kwa mja wewe johari,
Ka sabuni ya rohoni, povu lako liko wapi.

Ujima tumeusoma, shuleni tukamaliza,
Mengine tukahitima, walimu kutueleza,
Jahili na alosoma, kukupata atacheza.
Pesa ni mwana ukome, wahenga walisha nena.

Fukara hathaminiki, sababu ni yako wewe,
Warembo hatuwashiki, kukupata ni kiwewe,
Ka mimi siaminiki, jana nusu nizomewe,
Dinari huonekani, kukupata ni muhali.

*SOMO MOHAMED,*
*"SoMo De Prince tz",*
*Tanga-Tanzania.*

## Tusiharakishe shule

Yamesemwa mengi, nami langu naongeza,
Japo tone baharini, hakuna mbovu nyongesa,
Shule sikimbilieni, kufungua kwenye giza,
Tufunike kombe kwanza, mwanaharamu apite.

Tokea shule kufungwa, korona 'lidhibitiwa,
Hatua iliyoungwa, mkono 'poangaziwa,
Wana wetu walikingwa, na korona 'nye ukiwa,
Tufunike kombe kwanza, mwanaharamu apite.

Siichezeni karata, kuishi kuna nafasi.
Tajipanga bila tata, kwa mengi yaso mkosi,
Kamba 'liyeshaikata, vyeti vyake si ukwasi,
Tufunike kombe kwanza, mwanaharamu apite.

Stadi za maishani, wana waonyeshwe fika,
Maadili wafunzeni, wawe waja 'loongoka,
Utu mkiwajazeni, migogoro tatutoka,
Tufunike kombe kwanza, mwanaharamu apite.

Mirundikano ya wana, isubiri tujipange,
Madhara 'liyo mapana, ya korona tuyagange,
Takapoandaa vyema, tafungua kwenye mwanga,
Tufunike kombe kwanza, mwanaharamu apite.

*AUGUSTINE KIRIMI MIRITI,*
*Chuo Kikuu Kishiriki cha Tharaka,*
*Tharaka Nithi.*

## Afrika Inalia

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Wanaadamu wa leo, wayapitia machungu
Nawapa sababu leo, fahamu si yenu mbingu
Afrika hivi leo, inalia kwa uchungu.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Kokote mnakoenda, mwawachia milioni
Maabadini mwapenda, baraka kuzipateni
Kumbe nyoyo zinavunda, maovu mlotendeni.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Mwahusika vifo vingi, ila kesi mwakwepeni
Mnazoa sifa nyingi, mkishaachiliweni
Kuzibia mambo mengi, hongo mlipeaneni.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Mwatuzia vitu feki, vizuri kuchukueni
Magonjwa yanatukiki, mfanowe saratani
Mengineyo ni lukuki, hayatajiki jamani.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Tunazidi kuzozana, uchaguzi kijongea
Panga tunashikiana, kuua kujitolea
Polisi fahamiana, risasi kutugotea.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Badala kuleta sera, kampeni huwa hela
Kutugawieni gora, mwatunaseni po jela
Wasojua ni ukora, huo mnatukolela.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Wananchi tenganisha, nyinyi mkiunganika
Ukabila kudumisha, mataifa kuchafuka
Vizazi kuimarisha, vyenu vyeo kuvipaka.

Wanasiasa wa leo, mmeshakuwa miungu?
Jitwalia bilioni, pasipokuwa uwazi
Kandarasi kujipeni, kutukamua mavazi
Kodi kulazimisheni, natua Mpelelezi.

*MUKOYA H. AYWAH,*
*"Malenga Mpelelezi,"*
*Lang'ata, Nairobi.*

**KUWASIALIANA**

**Tutumie shairi lako kwa kuandika kwa Mhariri, Taifa Leo, S.L.P, 49010 Nairobi 00100 ama tuma barua pepe (e-mail) kwa taifa@ke.nationmedia.com Jumuisha jina lako na anwani.**

Tunapokea mashairi ya kati ya beti tano (5) na nane (8). Andika majina yako kamili, jina la ushairi na anwani yako.

Nation Media Group "Digital Copy"

EKALAKALA, MASINGA

# Pasta 'amgota' jombi aliyevuta fegi karibu naye

KISANGA kilizuka hapa jombi alipozabwa kofi na pasta kwa kuvuta sigara nyumbani kwake.

Duru zinaarifu kwamba jamaa alifika kwa pasta asubuhi na mapema kwa kazi ya kibarua. Jombi alipokuwa akimsubiri pasta arauke, aliwasha sigara yake na kuivuta bila kujali.

Inasemekana mtumishi wa Mungu aliponusa harufu ya sigara, aliamka mara moja. Alipigwa na mshangao alipompata jamaa akivuta sigara karibu na mlango wa nyumba yake na akamfokea vikali kwa kutomheshimu.

"Kwa nini unavuta sigara hapa kwangu. Mimi sipendi tabia hii hata kidogo. Kama unataka kuvuta sigara rudi kwako. Umeniudhi sana na hakuna kazi yako. Kwenda kabisa," pasta alimwambia jamaa. Jamaa alizusha na kuapa kutoondoka bila kufanya kazi ili apate riziki yake ya kila siku na ikabidi pasta amfukuze.

*Na John Musyoki*

## Wazo Bonzo




# Demu akataa sifa za kumtema mumewe

KABIANGA, KERICHO

**DEMU** wa hapa alimzushia dada yake aliyempongeza kwa kumtema mumewe.

Duru zinaarifu kuwa kidosho alikosona na mumewe wakagombana hadi akaamua kurudi kwa wazazi wake.

Siku mbili baada ya kufika nyumbani mrembo alitembelewa na dadake aliyeolewa kwingine na akamwambia kuwa alikuchukua hatua inayofaa.

" Ni vizuri umemtupa huyo mlofa aiyefaa kitu. Usitie guu huko tena. Ni vyema kama ungepata mume kama wangu," dada alimshauri.

Hata hivyo, kidosho alimjibu kwa ukali.

" Sitaki uchochezi wako. Hata hasira zimepoa, nitarudi kwa mpenzi wangu kesho," kidosho alimzushia dadake.

*Na Nicholas Cheruiyot*

# Boda azabwa kwa kuiba sanitaiza

CHEPALUNGU, BOMET

Bodaboda waliokuwa na ghadabu walimshika kwa nguvu mwenyekiti wa chama chao na kutisha kumwadhibu wakimlaumu kwa kuficha sanitaiza alizopewa na shirika moja awagawie.

Duru zasema kuwa hali ilikuwa shwari kwenye steji ya pikipiki huku wahudumu wakisubiri wateja na kubadilishana mawazo kuhusu hali ngumu inayotokana na corona.

Ghafla, mmoja wao alifichua kuwa kinara wao alipewa lita kadhaa za sanitaiza ili awagawie lakini yeye hakupata hata tone moja. Inasemekana alienda na kumkabili jamaa huyo.

"Iweje uliwapa watu sanitaiza na kuniweka pembeni hivyo! Unataka afya yangu iwe hatarini ili ufaidi nini? Acha uchoyo bwana," mwanabodaboda alisema kwa uchungu.

"Ona huyu! Ulikuwa wapi nikiwapa watu wote sanitaiza za bure. Kama unataka kunitoa uongozini mwa chama cha waendeshaji pikipiki jitayarishe kwa kivumbi cha siasa wakati huo ukifika," kinara alisema na kutoa kicheko cha dharau.

Inasemekana walianza kugombana na wanabodaboda wakashangaa kujua kulikuwa



na sanitaiza walizopaswa kupata lakini hazikuwafikia.

"Yaani ulipewa mitungi ya sanitaiza na ukaamua kuficha ili tukabiliane na hali yetu hivi! Kwanza ni lini ulichaguliwa kuwa kiongozi wetu? Leo utajua sisi si wa kuchezewa shere," mmoja alinguruma akimkaribia mwenyekiti huyo.

Mdaku anasimulia kuwa kinara huyo alipanda pikipiki yake na kuingurumisha tayari kuondoka kuhepa wenzake lakini akalazimishwa kushuka mara moja.

"Walimshika na kumsukuma hadi kwake ambapo walipata mitungi ya sanitaiza. Akiteteme-ka, aliomba msamaha na kuwataka wachukue kila kitu ili abaki kwa amani," mdaku alieleza.. Wanaboda boda hao waliondoka huku wakiapa kutokubali kuongozwa na mwizi.

*Na Nicholas Cheruiyot*

# Pasta akiona kwa kudai zaka kwa simu

KAGANDA, MURANG'A

**PASTA** wa kanisa moja eneo hili alipuuzwa na wafuasi wake alipoanza kuwapigia simu wakiwa majumbani kwao kuwadai sadaka.

Hii ni baada ya washiriki kukosa kuweka ahadi yao na mtumishi ya kuendelea kutoa sadaka wakilalamikia hali ngumu ya maisha. Kulingana na mdokezi, pasta alizuru kila boma la mshiriki baada ya sheria ya kutofanya ibada makanisani kuidhinishwa akiwakumbusha kuwa walifaa kutuma sadaka zao wakiwa nyumbani ili kuendeleza kazi ya injili.

Hatua ya pasta haikufurahisha waumini kwani waliunda kikundi kwenye mtandao wa WhatsApp na wakamsuta kwa akiwarai waendelee kutuma sadaka.

Baada ya majadiliano ya muda, washiriki waliamua kutotoa chochote wakidai kuwa pasta alikuwa mzembe. Juzi aliamua kupigia simu kila mshirika kumtaka atimize ahadi, nao wakampuuza.

*Na Leah Makena*

## Vituko vya Pokoyoyo

Na Wycotie···



Barua zote kwa Mhariri lazima ziwe na jina kamili la mwandishi na anwani yake. Zitumwe kwa: Mhariri, Taifa Leo, S.L.P. 49010, GPO 00100, Nairobi au tumia simu kutuma barua yako isiyopungua maneno 100 kwa nambari 20684 au barua pepe taifa@ke.nationmedia.com

# Corona haipaswi kutusahaulisha kuhusu kero la dawa za kulevya

WAKATI ambapo juhudi na rasilimali nyingi zinaelekezwa katika vita dhidi ya janga la Covid-19 jamii haifai kusahau kero la matumizi ya dawa za kulevya na pombe haramu miongoni mwa vijana.

Utafiti ulioendeshwa na Mamlaka ya Kupambana na Mihadarati na Vileo (Nacada) watoto wa kati ya umri wa miaka 10 na 24 huwa wameanza kutumia dawa za kulevya na pombe.

Idadi kubwa ya vijana hawa ni wale ambao wakati huu wako nyumbani baada ya serikali kufunga shule kufuatia mlipuko wa homa hii nchini mnamo Machi 13, 2020.

Kwa hivyo, wazazi na maafisa wa usalama wanapaswa kuwa waangalifu mno wakati huu ili kuzuia visa vya matumizi ya mihadarati miongoni mwa vijana.

Na wale ambao watapatikana kujiingiza katika uraibu huu wanafaa kupewa ushauri nafasa.

Wapelekwe katika vituo maalum vyenye washauri waliohitimu katika kazi huu.

*LILIAN OWAGA, Kericho*

## Kagwe alainishe wizara

JUZI, Waziri wa Afya Mutahi Kagwe kwa mara nyingine aliapa kupambana na maafisa wafisadi katika makao makuu ya wizara hiyo, Jumba la Afya, Nairobi.

Inasikitisha kuwa wakati kama huu wa janga la virusi vya corona wizara iliyoko mstari wa mbele katika vita vya kuzuia kuenea kwavyo inanyooshewa kidole cha lawama kwa uovu kama huo.

Hii ni kwa sababu kiasi kikubwa cha mabilioni ya fedha ambazo serikali ya Kenya imepokea kutoka kwa wahisani kufadhili mipango ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo zitakuwa zikisimamiwa na wizara hii.

Natoa wito kwa Waziri Kagwe kuwachukulia hatua kali maafisa wa wizara hii ambao itabainika kuwa wamepotoka kimaadili kiasi cha kuiba au kufuja fedha za umma.

*ESIRA JOSEPH, Uasin Gishu*




## Jumbe za corona ziwekwe pia kwenye barabara za miji

SERIKALI imekuwa ikipitisha habari kuhusu Covid-19 kupitia kwa vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Lakini ni muhimu kwa serikali pia kusambaza habari hizo katika barabara za miji na mitaani ili kuhakikisha kuwa jamii zisizo na makao zinafikiwa na jumbe hizo.

Watoto ambao hurandaranda barabarani na mitaani, maarufu kama chokoraa, pia wako katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huu.

Lakini inasikitisha kuwa wengi wao hawana makazi na hawawezi kupata maji safi, barakoa n ahata sanitaiza.

Na kwa sababu watu kama hawa wanaishi katika mazingira machafu serikali inapasa kuhakikisha kuwa inawafikia sio kuwapa habari pekee, bali iwape vifaa vya kujikinga.

*ALLAN KARIUKI, Nyeri*

## Nashukuru UhuRaila kwa kuweka nidhamu vyamani

RAIS Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga wamefanya vizuri kutokana na hatua yao ya kuweka nidhamu katika vyama vyao ikizingatiwa kuwa vyama vya Jubilee na ODM ndivyo vina idadi kubwa ya wajumbe katika bunge la kitaifa na seneti.

*MSOMAJI, Langata, Nairobi*

## Mahindi yasiagizwe toka nje

NAPINGA kabisa mpango wa serikali ya kuagiza magunia milioni nne ya mahindi kutoka ng'ambo eti kufikia uhaba wa zao hilo nchini.

Ukweli ni kwamba serikali ikifanya uchunguzi wa kina hapa kwetu kaunti ya Trans Nzoia na kaunti jirani ya Uasin Gishu, itabaini kuwa wakulima bado wana magunia mengi ya mahindi katika maghala yao. Kile ambacho kinasababisha dhana ya kutokuwepo kwa mahindi tosha nchini ni kwamba mwishoni mwa mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu, wakulima wengi hawakuuza mahindi kwa Bodi ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao (NCPB).

*NANCY NANJALA, Endebess, Trans Nzoia*

## Pesa za michezo zirejeshwe

NAKUBALIANA na pendekezo la Wizara ya Elimu kwamba shule za msingi na za upili humu nchini zinapasa kurejesha fedha ambazo zilitengwa kufadhili shughuli za michezo.

Hizi ni zile pesa ambazo zilinuiwa kufadhili fani mbalimbali za michezo katika mihula ya kwanza na ya pili.


Lakini baada ya shule kufungwa mapema mwezi Machi kufuatia mlipuko wa virusi vya corona nchini kulisitishwa shughuli zote za masomo zikiwemo zile za masomo. Kwa hivyo, walimu wakuu wanapaswa kurejesha fedha hizo za michezo ili zielekezwe katika shughuli zingine muhimu.

*DAMSON ONGER, Siaya*

## Fumbo

**KULIA:**
1. Tembo.
6. Aina mojawapo ya madini yenye thamani kubwa.
8. Jina linalotumiwa kwa "pesa" kuhusiana na uchumi.
9. Kati.
10. Hali ya mtu kupendelea kabila lake.
11. Ukoo.
12. Sehemu moja ya mji au wilaya.
17. Kualikwa.
20. Jina la heshima linalotumiwa kwa mwanamume.
22. Hali au kazi ya kuwa raisi wan chi.
23. Paka.

**CHINI:**
1. Hali iliyo bora au nzuri zaidi.
2. Sawa na kusema "ondosha".
3. Kifaa cha kufagilia.
4. Enea kila mahali.
5. Uchokozi.
7. Msitu.
13. Bashiri.
14. Haiji ila kwa ncha ya upanga.
15. Tumainia.
16. Endesha au ashikilia usukani wa uongozi wa serikali ya nchi.
18. Shughuli ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.
19. Ingiwa au patwa na hofu.



**KULIA:**
1. Mteja
6. Jirani
8. Ajizi
9. Muuza
10. Alinipa
11. Ibia
12. Uteo
17. Wanafaa
20. Ngoma
21. Ahadi
22. Mkwasi
23. Onana

**CHINI:**
1. Maafa
3. Eliki
3. Abiria
4. Ujamaa
5. Angani
7. Rauni
13. Tunuka
14. Okoka
15. Mwalia
16. Unyago
18. Fuata
19. Akiba

## Ujumbe Mfupi

**MAONI: ZAIDI** ya watu 300 jana waliripotiwa kuhudhuria hafla moja ya mazishi katika Kaunti ya Nyeri, jambo ambalo ni kinyume na kanuni zilizowekwa na serikali kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona. Miongoni mwa waliohudhuria ni wanasiasa na watu maarufu serikalini. Je, unahisi kwamba kuna mapendeleo katika utekelezaji wa kanuni hizo?

Unatarajia raia kufuata sheria wakati watunga sheria wanakwepa? Wao ndio wanasambasa virusi vya corona si raia. Jambo hili linatufanya kuhisi kuwa hakuna Covid-19. Kuna mwanasiasa yeyote aliyeambukizwa na akafariki?

***Pst Godfrey Sambia***

Kwenye picha ni dhahiri hao watu hawajavunja sheria. Wacheni maneno za chuki kuhusu virusi vya corona. Watu wa familia wakiwa zaidi ya kumi na tano, watatoroka nyumbani siku ya mazishi waende wapi?

Japheth Muturia Muriungi

Nadhani kufikia sasa kila Mkenya anaelewa barabara virusi vya corona ni nini, husambazwa kivipi na madhara yake ni yapi. Licha ya kutoa kanuni zitakazofutwa kudhiti kusambaa kwa Covid-19, si rahisi serikali kuwa katika kila hafla kuhesabu waliohudhuria ili kubaini ikiwa kanuni zilikiukwa au la.

***Peter Onesmus***

Ndio maana hivi vita dhidi ya Covid19 kuvishinda itakuwa vigumu sana, kwa kuwa tuna mazoea ya kupuuza kila jambo. Vyombo vya usalama, machifu na wakuu wa nyumba kumi hufanya kazi gani?

***Bahati Okunu***

Tuna sheria mara mbili: moja ni yetu na nyigine ni ya wao wanasiasa. Ole wetu.

Anthony Wachira Ndung'u

Mnyonge hana lake! Watu wa haiba kubwa na maeneo yao wanapendelewa kufanya watakavyo!

***Francis Omuleli, Molo***

Kenya kuna sheria ya wananchi na wenye nchi.

Joyfa Weaver

Heri sisi Wakenya tutoke tufanye kazi maana mimi sioni hii serikali inaongea nini. Tunafungiwa manyumba huku Nairobi, tunatutwa kazi, tunawekewa lockdown Nairobi hakuna chakula hatuezi enda nyumbani. Si angeweka kafyu saa 11 jioni lakini atoe lockdown?

***Samweli***

Wanajihesabu kama hawana virusi vya corona ni kana kwamba wanangoja dalili. Kuna watu ambao hawaonyeshi dalili zozote. Nitajitenga na watu kama hao kwa majuma mawili.

***Peter Langat***

Bila shaka sheria ya Kenya sio msumeno unaokata kuwili bali ni upanga tu. Zimewekewa walalahoi.

***Virgil Peter Emusugut***

Hili nì swali balagha kwa sababu nyie mwaelewa kuhusu 'shamba la wanyama.'

Peter Pound

Kuna mapendeleo lakini virusi vya corona havitapendelea.

***Shadrack Meeme Lunge***

Sheria ziliwekwa kweli kuhusu hafla kama iliyofanyika Nyeri. Ni makosa na hiyo nikuonyesha mapendeleo kwa upande wa serikali na wanasiasa nao ndio wao wanatengeneza sheria bungeni lakini hawataki kuzizigatia!

***John Kaara, Mombasa***

Ndio kuna mapendeleo. Hii ndiyo kawaida ya Wakenya wenye mali huwa hawatii sheria.

***Imbai Nickson***

Licha ya kwamba zinguo la mtukufu ni ufito, kuna utepetevu katika kuwaadhibu watu wa hadhi ya juu wavunjapo sheria.

***Milton Amerigo, Mwatate***

Kanuni zilizowekwa kuhusiana na kudhibiti virusi vya corona ni kigezo cha kukandamiza mwananchi wa kawaida. 'Wenye nchi' hawajakoma shughuli zao za kawaida.

***Stephen Njuguna***

Kenya iko na wenyewe

***Duncan Mc Onyango***

**MJADALA WA LEO:** Hapo jana Rais Uhuru Kenyatta alionekana kuzima matarajio ya Wakenya kuhusu kumaliza kafyu. Aliongeza muda wa kafyu kwa mwezi mmoja zaidi na kubadili saa kuwa kuanzia saa kumi alfajiri hadi saa tatu usiku. Je, hisia zako ni zipi kuhusu hatua hiyo ya rais? Ukifafanua sababu zako, je, unamuunga mkono Kiongozi wa Taifa au la?

**KUWASILIANA**

Tutumie maoni yako kuhusu mjadala huu kwa nambari ya simu **20684** au barua pepe **taifa@ke.nationmedia.com** na tutachapisha kesho baadhi ya maoni tutakayopokea.

Nation Media Group "Digital Copy"

JAMVI

# Vigogo wa BBI walenga kuvuruga Mudavadi kwa kusita kusakata densi yao

Na CHARLES WASONGA

MISUKOSUKO inayoshuhudiwa wakati huu katika siasa za Magharibi mwa Kenya inatishia kuvuruga mipango ya Ford Kenya na Amani National Congresss (ANC) kuungana kwa ajili ya uchaguzi wa 2022.

Ishara ya hali hiyo ni jaribio la kumng'oa mamlakani kiongozi wa Ford-Kenya Moses Wetang'ula wiki jana, hatua inayofasiriwa kama inayolenga kulemaza safari ambayo mwenzake wa ANC Musalia Mudavadi ameanzisha kuingia Ikulu 2022.

Mapinduzi hayo, ambayo yamepigwa breki kwa muda na msajili ya vyama vya kisiasa Anne Nderitu, yanaongozwa na Katibu Mkuu wa Ford Kenya Eseli Simiyu, Mbunge wa Kanduyi Wafula Wamunyinyi na Gavana wa Bungoma Wycliffe Wangamati.

Wadadisi wanasema japo Wetang'ula ndiye analengwa kupokonywa wadhifa wake wa kiongozi wa chama hicho cha Simba, kichocheo, haswa, cha

ENDELEA UK 12

>> Ndani

Ruto kulazimika kubadili mikakati yake ya siasa baada ya Uhuru kumvuruga UK 14

Nation Media Group Digital Copy

TAIFA Jumapili

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

# Tukatae uzembe wa viongozi wetu

Nl aibu kubwa kusikia kuwa kuna kaunti kadhaa ambazo hazijachukulia janga la corona kwa uzito unaostahili.

Kaunti hizo hazijajiandaa kikamilifu kupambana na janga hili, ilhali idadi ya wagonjwa nchini inaongezeka kila kukicha.

Tangu mgonjwa wa kwanza wa virusi vya corona alipotangazwa nchini takriban miezi mitatu iliyopita, tulianza kuona viongozi mbalimbali wakijikakamua kujiandaa kwa mkurupuko.

Inasikitisha tunapopokea ripoti kuwa baadhi ya kaunti zingali na vitengo duni vya kulaza wagonjwa wa Covid-19 na endapo zitakumbwa na mkurupuko mkubwa, kutakuwa na janga tutakalojutia kama taifa.

Kwa muda mrefu sasa, vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti kuhusu kaunti ambazo zinajitahidi kuepusha janga aina hiyo, na vile vile, kutangaza kuhusu kaunti ambazo bado ziko nyuma.

Ripoti hizi huwa zimenuiwa kuhimiza viongozi wa maeneo husika wakaze kamba ili taifa lote lisonge mbele kwa mwelekeo mmoja wakati tunapojikakamua kupambana na ugonjwa huu hatari.

Magavana wa kaunti zilizozembea lazima wajifunze kutoka kwa wenzao ambao wamebobea katika maandalizi ya kuboresha vituo vya afya vinavyotumiwa kutibu wagonjwa wa Covid-19.

Sababu ambayo baadhi yao wamekuwa wakitoa mara kwa mara, kwamba Serikali Kuu haijawatumia fedha, haina msingi kamwe.

Tuna hakika mamilioni ya pesa zingepatikana kama tungekuwa tunazungumzia maandalizi ya makongamano katika hoteli za kifahari ambapo maafisa wanaohudhuria hulipwa marupurupu tele kila siku.

Wakati huu ambapo safari nyingi za ndani na nje ya nchi pamoja na mikutano imepigwa marufuku, viongozi wa kaunti wangetarajiwa kutumia mamlaka yao kuunda bajeti za ziada kwa minajili ya kutenga pesa za kutosha za kupambana na corona.

Vile vile, kiongozi bora ni yule ambaye ana uwezo wa kutafuta ushirikiano kutoka kwa asasi nyinginezo kitaifa na kimataifa hasa ifikapo katika masuala ya kuokoa maisha ya wananchi.

Uzembe huu wa viongozi wa kaunti kurusha lawama kwingine kila mara wanaposhindwa na kazi zao haufai kuvumiliwa.

Ni sharti wananchi wazinduke na waitishe huduma bora kutoka kwa viongozi wao wote bila kukubali kuhadaiwa kila mara.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
Mkurugenzi Mkuu: STEPHEN GITAGAMA
Mkurugenzi wa Uhariri: MUTUMA MATHIU
Mhariri : PETER NGARE

**Nukuu ya wiki**

**"Nataka ieleweke wazi kuwa Idara ya Mahakama ni huru kikatiba, na huwa haipokei maagizo wala kupata mamlaka yake kutoka kwa Serikali Kuu."**

Jaji Mkuu David Maraga

**Kivumbi** Mpango pia upo wa kuzuia ANC na Ford-K kuungana



Kiongozi wa chama cha Ford-Kenya Moses Wetang'ula (kushoto) na Mbunge wa Kiminini Chris Wamalwa, kwenye kikao wiki iliyopita. *Picha/Maktaba*

# Mudavadi alengwa kwa kusita kupigia BBI debe

KUTOKA UK 11

mapinduzi hayo ni hatua ya Mudavadi kukataa kujiunga na Mpango wa Maridhiano (BBI).

Mvumishaji mkuu wa wimbi hili katika eneo la Magharibi ni Katibu Mkuu wa Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Nchini (COTU) Francis Atwoli.

Bw Atwoli Amekuwa mkereketwa mkuu wa mchakato wa BBI ulioasisiwa na Rais Uhuru Kenyatta na Kiongozi wa ODM

Katika siku chache zilizopita, Bw Mudavadi amekuwa akifanya mikutano kadhaa na wanasiasa kutoka vyama na maeneo mbalimbali nchini afisini mwake katika mtaa wa Lavington na hoteli za Nairobi.

Miongoni mwa wanasiasa hao ni Kiongozi wa Narc Kenya Martha Karua, Gavana wa Uasin Gishu Jackson Mandago, Seneta wa Kiambu Kimani Wamatangi, aliyekuwa mbunge wa Gatanga Peter Kenneth na aliyekuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma Dkt Sally Kosgei.

**Mapinduzi Ford-Kenya**

Wengine ni wabunge wa kutoka eneo la magharibi ambao ni wandani wa Naibu Rais William Ruto Didmus Barasa (Kimilili), John Waluke (Sirisia) na Benjamin Washiali (Mumias Mashariki), miongoni mwa wengine.

Mikutano hii ya Mudavadi, inasemekana kumkera Bw Atwoli na wakereketwa wengine wa BBI kutoka magharibi mwa Kenya, ambao wanamwona kiongozi huyo wa ANC kama ambaye anasuka mpango wake wa kisiasa nje ya mwavuli wa BBI.

"Mudavadi anafahamu hilo na ndio maana juzi alimlaumu Mzee Atwoli akidai ndiye alidhamini jaribio la mapinduzi dhidi ya Bw Wetang'ula. Vile vile, amemlaumu Bw Odinga kwa vuta nikuvute hiyo ya uongozi ndani ya Ford Kenya," anasema mchanganuzi wa masuala ya kisiasa Martin Andati.

"Mapinduzi ndani ya Ford Kenya yalipangwa na kutekelezwa kwa lengo la kunitisha mmi pamoja na ndugu yangu Wetang'ula. Maovu haya yamedhaminiwa na Atwoli kunimaliza kisiasa. Mzee Atwoli anashirikiana na kiongozi wa mojawapo ya vyama tanzu vya muungano wa NASA ambaye lengo lake kuporomosha na kudhibiti wengine kisiasa," akasema Bw Mudavadi.

Ni wazi kuwa Bw Mudavadi alikuwa akimrejelea Bw Odinga.

Kulingana na Bw Andati, madai ya Bw Mudavadi, yaliyoshadidiwa baadaye na Bw Wetang'ula yana mashiko ikizingatiwa kuwa kabla ya jaribio hili Dkt Eseli na wenzake walimtembelea Bw Odinga afisini mwake katika jumba la Capitol Hill, Nairobi.

"Isitoshe, mkutano wa wajumbe wa Ford Kenya walioidhinisha kung'olewa kwa Wetang'ula ulipangwa haraka na kuendeshwa baada ya mkutano wa viongozi wa magharibi ambao ulifanyika nyumbani kwa Bw Atwoli katika Kaunti ya Kajiado," anaongeza.

Ni katika mkutano huo wa Kajiado ambapo Gavana wa Kakamega Wycliffe Oparanja na Waziri wa Ugatuzi Eugene Wamalwa walitawazwa kama viongozi ambao wataongoza ajenda ya maendeleo ya eneo la Magharibi mwa Kenya katika ngazi ya kitaifa.

"Oparanya na Wamalwa ndio watawakilisha eneo letu katika mchakato wa BBI ili tuweze kuchuma matunda yatakayotokea, haswa katika serikali itakayobuniwa baada ya uongozi wa sasa kukamilisha kipindi chake cha pili," akasema Bw Atwoli baada ya mkutano huo uliohudhuriwa na zaidi ya viongozi 40.

Lakini kwenya mahojiano Alhamisi, Katibu huyo Mkuu wa COTU alijitenga na madai ya kudhamini jaribio la mapinduzi dhidi ya Bw Wetang'ula ua njama za kumhujumu Bw Mudavadi kisiasa.

Alisema Kiongozi huyo wa ANC angali kiongozi wa kisiasa wa jamii ya Waluhya na jamii zingine za eneo la Magharibi mwa Kenya kama vile Wateso na Wasabaot.

"Sina uhasama wowote na Mudavadi. Yeye ndiye amekuwa kiongozi wa kisiasa wa jamii ya 'Mulembe' tangu Aprili 4, 2016 tulipomtawaza katika uwanja wa Bukhungu, mjini Kakamega. Hilo halijabadilika. Kazi ya Eugene na Oparanya itakuwa kutetea eneo letu katika masuala ya maendeleo katika ngazi ya Serikali Kuu," Bw Atwoli akafafanu.

Dkt Eseli pia amepuuzilia mbali madai ya Mbw Mudavadi na Wetang'ula akidai mkutano wao na Bw Odinga ulijadili changamoto zinazokumba Chuo Kikuu cha Kibabii.

"Uamuzi wa wanachama wa baraza kuu (NEC) ya Ford Kenya wa kumwondoa Wetang'ula unachangiwa na utepetevu wake. Chini ya uongozi wake chama chetu kimepoteza umaarufu na wanachama wengi. Hatuchochewi na Raila au Atwoli kwa sababu wao sio wanachama wa Ford Kenya," akasema Dkt Eseli kwenye mahojiano na "Jamvi la Siasa".

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi Herman Manyora pia anaungamna kuwa Bw Mudavadi anahujumiwa kisiasa kwa sababu anaonekana kukaidi mwelekeo wa kisiasa wa Rais Kenyatta na Bw Odinga chini ya mwavuli wa BBI.

Mchanganuzi huyu anasema misukosuko ndani ya vyama vya kisiasa nchini ni jambo la kawaida na kwamba "Mudavadi na Wetang'ula wasiwe waoga na kulia kila wakati".

"Hii sio mara ya kwanza kwa mapinduzi kama hayo kutokea katika chama cha Ford Kenya, ANC na sasa yanaendelea katika chama tawala cha Jubilee kinachoongozwa na Rais Kenyatta," anaeleza mhadhiri huyu.

Ili kutolea maoni habari hii, nenda kwa taifaleo.nation.co.ke

# Uhuru akanganya wanasiasa kwa karata wasioelewa

Na WANDERI KAMAU

RAIS Uhuru Kenyatta anaendelea kuwashangaza wengi kuhusu karata anayocheza kwenye urithi wake hapo 2022, ikiwa si dhahiri hadi sasa kuhusu kiongozi anayempendelea kuwa mrithi wake.

Katika siku za hivi karibuni, Rais Kenyatta amekuwa akikutana, kucheka na hata kutangamana na viongozi wakuu wa siasa nchini, hali ambayo wadadisi wanasema huenda imewaacha kwenye njiapanda.

Kufikia sasa, wale wanaoonekana kuwa wagombea wakuu wa wadhifa huo ni Naibu Rais William Ruto, kiongozi wa ODM Raila Odinga, kiongozi wa chama cha Amani National Congress (ANC) usalia Mudavadi, Seneta Gideon Moi (Baringo) na kiongozi wa Wiper Kalonzo Musyoka.

Tangu kubuni handisheki na Rais mnamo Machi 2018, Bw Odinga amekuwa akifasiriwa kuwa kiongozi anayependelewa na Rais Kenyatta kuwa mrithi wake kutokana.

Upeo wa ukaribu wao ulikuwa mnamo Jumanne wiki hii, ambapo wawili hao walinaswa kwenye video wakisafiri kwenye gari moja jijini Nairobi usiku, duru zikieleza walikuwa wakikagua miradi inayoendeshwa na Baraza Jipya la Kusimamia Jiji (NMS).

Mnamo Jumatatu, kwenye sherehe za Sikukuu ya Madaraka katika Ikulu ya Nairobi, Rais Kenyatta na Dkt Ruto walionyesha ukuruba wa karibu, huku hata wakivalia mavazi yaliyofanana. Hili ni licha ya uhusiano wao unaoonekana kudorora kila siku.

Mnamo Desemba mwaka uliopita, Rais Kenyatta alisafiri pamoja na Bw Mudavadi kwenye ndege yake rasmi katika hafla ya kijeshi mjini Garissa, hali iliyoibua maswali kwamba huenda anamjenga Bw Mudavadi kuwa mrithi wake.

Mapema mwezi uliopita, Chama cha Jubilee (JP) kilibuni mkataba na Kanu, hali iliyofasiriwa kama njia ya Rais Kenyatta kumwandaa Seneta Moi kuwa mrithi wake, ili "kurejesha mkono" kwa familia ya Mzee Daniel Moi.

Mzee Moi ndiye aliyemwidhinisha Rais Kenyatta kuwa mgombea wa urais wa Kanu mnamo 2002, baada yake kustaafu rasmi kama rais.

Na baada ya mkataba ya Jubilee na Kanu, Bw Musyoka alisema kuwa Wiper imempa kibali kuanza mazungumzo na Rais Kenyatta kuhusu uwezekano wa kubuni muungano kama huo.

### Ataunga nani mkono?

Na kufuatia mwelekeo huo, wadadisi wa siasa wanasema kuwa ingawa nia ya Rais Kenyatta ni kuwaleta wanasiasa wote kwenye kapu moja, anafahamu lengo lake la mwisho.

Kwenye mahojiano, Prof Macharia Munene, ambaye ni mchanganuzi wa siasa, anamtaja Rais Kenyatta kama mwanasiasa mjanja, anayefahamu kwa undani kuhusu karata anayocheza.

Hata hivyo, anawataja wanasiasa wengine, hasa Mabw Odinga na Ruto, kama wanasiasa werevu pia, ikizingatiwa wote walilelewa kisiasa na Mzee Moi.

"Rais Kenyatta alilelewa kisiasa na Mzee Moi. Hivyo, anafahamu kuhusu karata anayocheza. Yuko katika mazingira magumu, yanayomhitaji kuwa mwerevu sana. Walielewana na Bw Odinga kwa msingi wa kuleta utulivu wa kisiasa nchini, hivyo lazima ahakikishe kuwa hajamtenga kwa vyovyote vile. Pia, waliungana na Dkt Ruto kwa msingi wa 'deni' la kisiasa mnamo 2012. Hivyo, hawa ni kama watoto wawili ambao ni vigumu kuwatenga," asema Prof Munene.

Na ingawa taswira iliyopo ni kuwa Rais amekosana na Dkt Ruto, anasema kuwa itabidi Rais azime dhana hiyo kijanja, kwani kikatiba, Dkt Ruto bado ni naibu wake na mwanasiasa ambaye pia ni mwanafunzi wa Moi.

Wadadisi wanasema kuwa 2022 ingali mbali ambapo kama mwanasiasa, Rais Kenyatta anafahamu kwa undani kuwa wanasiasa wanaweza kubuni miungano licha ya tofauti zao.

"Huu ni mwelekeo tutamwona Rais akizingatia kwani anataka kubuni mazingira ambapo atatekeleza ajenda yake ya maendeleo huku akiangalia mbele kuhusu mchakato wa urithi wake," asema Prof Munene.

## Juhudi za awali kupatanisha Waluhya zimegonga mwamba mara kadhaa

# Atwoli atafanikiwa kuunganisha nyumba pana ya 'Mulembe'?



Kiongozi wa chama cha Ford-Kenya Moses Wetang'ula (kushoto) na Mbunge wa Kiminini Chris Wamalwa, kwenye kikao wiki iliyopita. *Picha/Maktaba*

Na CHARLES WASONGA

KWA mara nyingine Katibu Mkuu wa Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Nchini (COTU) Francis Atwoli amefufua juhudi za kuunganisha jamii ya Waluhya.

Lakini swali ni je, wakati huu afaulu au la?

Hii ni baada ya majaribio ya kufikia lengo hilo hapo nyuma kufeli kutokana na mseto wa sababu.

Uchunguzi umebaini kuwa baadhi ya sababu kuu zilizolemaza juhudi hizo ni ukosefu wa kiongozi shupavu na jasiri anayeweza kubeba mwenge wa jamii hii na kuvumisha matamanio yake haswa katika nyanja za kisiasa na kiuchumi.

Aidha, wachanganuzi wanasema kuwa ubabe kati ya takriban jamii 17 ndogo ndogo zinazounda kabila la Abaluhya umefifisha juhudi za kupalilia umoja wake.

Historia ya siasa za jamii hii ya 'Mulembe' pia imeonyesha kuwa ukosefu wa wanasiasa wenye misimamo thabiti umechangia umoja wao kisiasa kuyumbishwa na wanasiasa wa makabila mengine.

Lakini kulingana na Herman Manyora na aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Butere Amukowa Anangwe, ukosefu wa dhana au sera mahsusi wa kuwaunganisha wanajamii wote 17 kutoka kaunti tano za watu wa asili ya kabila hili ni kikwazo kikuu.

"Licha ya hayo, sasa kuna matumaini makubwa kwamba Bw Atwoli atafaulu kuwaunganisha Waluhya wote kupitia mchakato wa maridhiano (BBI)," anasema Bw Manyora ambaye ni mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kulingana naye, ishara ya juhudi hizo kufanikiwa ni kile anachotaja kama kufanikiwa kwa mkutano wa viongozi wa Abaluhya ambayo Bw Atwoli aliandaa nyumbani kwake Kajiado juzi.

"Gavana wa Kakamega Wycliffe Oparanya na Waziri wa Ugatuzi Eugene Wamalwa, ambao waliteuliwa kuongoza ajenda ya maendeleo katika janibu za Waluhya wana tajriba kubwa katika ulingo wa siasa na serikali," anaeleza Manyora.

Kwa upande wake, Profesa Anangwe anampa shime Bw Atwoli aendeleze mchakato huo lakini anamshauri kujiondoa katika kivuli cha kiongozi wa ODM Raila Odinga.

"Atwoli aondoe dhana kwamba mipango aliyoanzisha inalenga kumsaidia Raila kuingia Ikulu 2022. Dhana hii inakolezwa na viongozi kama vile Musalia Mudavadi na Moses Wetang'ula," anaandika Profesa Anangwe, ambaye aliwahi kuhudumu kama Waziri katika Serikali ya Hayati Mzee Daniel Moi.

Kwenye kikao na wanahabari mtaani Karen, Nairobi juzi, Mbw Mudavadi na Bw Wetang'ila waliutaja mkutano huo kama "jukwaa la kuendeleza azma ya Bw Odinga ya kuingia Ikulu 2022".

"Hamna chochote cha kufaidi Waluhya kilijadiliwa kule. Jamii ya 'Mulembe' inafaa kukataa kabisa njama kama hizo za watu wachache kuwatumia kama ngazi ya kukwea mamlakani," akasema Bw Wetang'ula.

### Mila na desturi

Naye aliyekuwa Seneta wa Kakamega Bonny Khalwale, anasema kulingana na mila na desturi ya jamii hiyo ni mwiko kwa Mzee wa umri na hadhi ya Atwoli kuandaa mkutano wa jamii "nje na ya nyumba ya mke wa tatu."

"Mkutano kama huo unapasa kufanyika katika mojawapo ya kaunti zetu na baada ya ushauriano wa kina na viongozi wa matabaka mbalimbali wakiwemo wazee," anasema Dkt Khalwale.

Ni kwa misingi hiyo ambapo mwanasiasa huyu, ambaye ni mwandani wa karibu wa Naibu Rais William Ruto, anashikilia kuwa juhudi za sasa za Bw Atwoli zitafeli.

Itakumbukwa kuwa mnamo Aprili 2, 2016 Bw Atwoli alijaribu kuwaunganisha viongozi wa kisiasa kutoka ukanda wa Magharibi bila mafanikio.

Kilele cha juhudi hizo kilikuwa ni hafla ya kufana katika uwanja wa Masinde Muliro mjini Kakamega, ambapo Bw Mudavadi alitawazwa kuwa msemaji wa jamii ya Waluhya.

Bw Wetang'ula alidinda kuhudhuria sherehe shughuli hiyo.

Kabla ya kuandaliwa kwa hafla hiyo, Bw Atwoli alidai kudhamini utafiti kukadiria umaarufu wa viongozi wakuu kutoka jamii hiyo ambapo Bw Mudavadi alisemekana kubuka mshindi kwa kupata asilimia 39 akifuatwa na Bw Wetang'ula alipata asilimia 32.

Seneta huyu wa Bungoma alipuuzulia mbali matokeo ya utafiti huo ulioendeshwa na wasomi kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, akisema mradi huo ulilenga kumsawiri kama mwanasiasa "limbukeni".

Hayo yalijiri baada juhudi zingine ya kuunganisha jamii hiyo, zilizoongozwa na aliyekuwa Spika wa Bunge la Kitaifa Kennethe Marende kutibuka.

Wengine walioshiriki mpango huo uliolenga kutoa uhamasisho kwa jamii hiyo kuunga mkono chama kimoja cha kisiasa katika mchaguzi mkuu wa 2017 walikuwa Mudavadi, Waziri Wamalwa, aliyekuwa Mbunge wa Lugari Cyrus Jirongo na Waziri Msaidizi Ababu Namwamba.

Kwa mara nyingine mchecheto wa siasa za NASA ukiongozwa na Bw Odinga ulijiri na kuzamisha ndoto hiyo.

Na mapema mwaka huu, juhudi zilitajwa kama za kuunganisha eneo la Magharibi kiuchumi chini ya mwavuli wa Muungano wa Wabunge wa eneo hilo (WPC) pia ziyeyushwa na siasa za BBI.

Chini ya mwenyekiti wa WPC Sakwa Bunyasi, ambaye ni Mbunge wa Nambale, wabunge hao wandani wa Dkt Ruto walidai kulenga kuchochea ufufuzi wa viwanda vilivyoporomoka katika eneo hilo ili kutoa nafasi za ajira kwa wakazi. Walilenga kampuni ya sukari ya Mumia, ile ya Nzoia na kampuni ya karatasi ya Pan Paper iliyoko Webuye.

"Tunapania kuwakomboa watu wetu kiuchumi kwanza ndiposa tuwaunganishe kisiasa. Hii ndio azma yetu kuu," Bw Bunyasi akawaambia wanahabari katika mkahawa wa Serena, Nairobi alipotangaza kuwa wangesusia mkutano wa BBI uliooratibiwa kufanyika uwanjani Bukhungu, Kakamega Januari 18.

Baada ya juhudi hizi zote kufeli, Bw Manyora sasa ni mwingi wa matumaini kwamba harakati za sasa za Bw Atwoli zitazaa matunda chini ya mwavuli wa BBI na handisheki.

Lakini wadadisi wengine wanashikilia kuwa ndoto hii bado itakosa kutimia ikiwa viongozi wa Waluhya hawatazika hulka ya kutoaminiana kwa misingi ya makabila madogo wanakotoka.

Nation Media Group "Digital Copy"

Naibu Rais adhalalishwa na mkubwa wake kila upande na kuachwa akiwa hoi

# Kiboko cha Uhuru sasa kumlazimu Ruto kubuni mikakati mipya kisiasa

NA BENSON MATHEKA

BAADA ya miaka minane ya kujipiga kifua kwa kuthibiti chama cha Jubilee na kuungwa mkono na idadi kubwa ya wabunge wa chama hicho tawala, Naibu Rais William Ruto amelazimika kumeza kiburi chake, kufyata ulimi na kufuata nyayo za Rais Uhuru Kenyatta.

Idadi ya wabunge wanaomuunga mkono inaendelea kupungua na mamlaka yake yameshushwa na hivyo kumnyima ushawishi aliokuwa akifurahia.

Wadadisi wanasema Dkt Ruto alivuka mipaka kwa kupinga ajenda na maamuzi ya Rais na kutaka kuonyesha ubabe na umaarufu wake hata katika ngome ya kiongozi wa nchi.

Dkt Ruto amekuwa akitofautiana na Rais Kenyatta kuhusu vita dhidi ya ufisadi na Mpango wa Maridhiano (BBI) na kuonekana kuwa sauti upinzani ndani ya serikali.

"Amekunja mkia, amekatwa pembe zilizomfanya kumkaidi kiongozi wa nchi, amekatwa kucha zilizomfanya awe na makali na sasa ameanza kufuata nyayo," asema mdadisi wa siasa Geff Kamwanah.

Anasema kwamba Dkt Ruto alitenda dhambi kubwa za kisiasa kwa kuendelea na siasa, kutumia miradi ya serikali kujipiga kifua badala ya kumsifu kiongozi wa nchi, kufanya chama cha Jubilee kuwa mali yake, kukaidi na kudharau uamuzi wa kiongozi wa nchi..

"Hii ndio sababu Rais alianza kwa kumuonyesha kuwa ndiye kiongozi wa chama tawala cha Jubilee alipobadilisha wanachama wa kamati ya usimamizi bila kumhusisha Dkt Ruto, akaangusha mjeledi kurejesha nidhamu akiwalenga wabunge waliomuasi kwa kuelekeza uaminifu wao kwa Ruto kabla ya kupanga upya serikali yake na kufanya ofisi ya Naibu Rais kuwa idara katika ofisi yake," asema.

Baada ya kuthibiti chama, Rais Kenyatta aliita mkutano wa maseneta wa Jubilee na washirika wake katika ikulu kuwapa maagizo ya kuwabandua washirika wa Dkt Ruto kutoka uongozi wa Seneti na kamati zake.

Dkt Ruto ambaye anafaa kuhudhuria mkutano huo kama Naibu kiongozi wa chama na baadhi ya wandani wake waliususia.

"Kuvuliwa nyadhifa kwa wandani wake na kutishwa kuadhibiwa kwa washirika wake waliosusia mkutano huo kulimfungua macho Dkt Ruto. Aligundua kuwa hawezi kushindana na kiongozi wa nchi na ndio sababu hakusema chochote walipotemwa," asema mdadisi wa masuala ya siasa David Wanyama.

**AJENDA ZA RAIS**

Inasemekana kuwa Dkt Ruto aliwaambia wandani wake wakubali mabadiliko hayo.

Kulingana na Seneta Irungu Kang'ata wa Murang'a, mabadiliko hayo yalilenga wanachama wanaohujumu ajenda za Rais Kenyatta na handisheki yake na Kiongozi wa ODM Raila Odinga.

"Ikiwa hauungi mkono ajenda za Rais haufai kunufaika na wadhifa wowote kwa hisani ya chama," asema Bw Kang'ata.

Naye katibu Mkuu wa chama hicho Raphael Tuju asema bila nidhamu katika chama tawala hakuwezi kuwa na nidhamu katika serikali.



NAIBU Rais William Ruto. *Picha/Maktaba*

Kulingana na Bw Wanyama, ishara kwamba Dkt Ruto aligundua hana budi kufuata nyayo za Rais zilionekana kwenye hotuba ya Madaraka Dei.

"Alionekana mnyenyekevu tofauti na kabla ya Uhuru kuanza kuangusha shoka alipokuwa akizungumza kwa kiburi. Siku iliyofuata alihudhuria mkutano wa wabunge wa Jubilee katika Ikulu ambao wandani wake walivuliwa nyadhifa akishuhudia," asema.

Mdadisi huyu asema kuwa kuhudhuria kwake na wandani wake kulitokana na hofu ya kuadhibiwa. Kabla ya mkutano huo Bw Tuju alikuwa amedokeza kuwa huenda wakamchukulia Naibu Rais hatua za nidhamu kwa kile alichotaja kwenda kinyume na kanuni za chama.

Bw Kamwanah anasema kuwa Dkt Ruto hana budi kuunga ajenda za serikali hata kama shingo upande ikiwa atabaki katika Jubilee.

"Wandani wake wengi wameingiwa na baridi na kugeuza uaminifu wao kwa Rais Kenyatta. Amepokonywa mamlaka yaliyotwikwa ofisi ya Naibu Rais kwenye mabadiliko yaliyotangazwa Jumatano na kwa hivyo atakuwa akipimiwa hewa na ofisi ya Rais," asema.

Kwenye mabadiliko hayo, ofisi ya Rais haitakuwa na bajeti na itategemea pesa kutoka ofisi ya rais na wafanyakazi wataajiriwa na Tume ya Utumishi wa Umma.

Kulingana na Profesa Macharia Munene wa Chuo Kikuu cha Kimataifa Cha Amerika (USIU), Rais Kenyatta alitaka kudhihirishia Dkt Ruto na wandani wake kwamba ndiye aliye kwenye usukani.

" Wengi wa washirika wake wameingiwa na baridi. Ni wachache tu wanaopaza sauti kama Moses Kuria, Oscar Sudi, Samson Cherargei, Kipchumba Murkomen, Gladys Shollei, Susan Kihika na Ndindi Nyoro. Hata hivyo haujulikani wale wa kutoka Mlima Kenya watabaki naye hadi lini," asema Bw Wanyama.

# 'Masaibu' anayopitia Naibu Rais yaongeza umaarufu wake eneo la Mlima Kenya

NA WANDERI KAMAU

UMAARUFU wa Naibu Rais William Ruto unaonekana kuongezeka katika ukanda wa Mlima Kenya, licha ya juhudi zinazoendeshwa na Chama cha Jubilee (JP) kuwang'oa wandani wake kwenye nyadhifa mbalimbali katika Seneti na Bunge la Kitaifa.

Wenyeji wengi wanafasiri juhudi za kuwaondoa wandani hao kama "usaliti wa kisiasa" unaolenga kumzuia Dkt Ruto kuendelea kukita kambi kisiasa katika eneo hilo, anapopania kuwania urais 2022. Dkt Ruto amefanikiwa kujizolea ufuasi mkubwa katika ukanda huo kutokana na ziara na michango yake ya mara kwa mara, hasa katika makanisa, shule, makundi ya vijana na akina mama.

Pia ahadi za Rais Uhuru Kenyatta alipokuwa akifanya kampeni 2013 na 2017 kuwa atamuunga mkono 2022 zimefanya wakazi wengi kusisitiza kuwa sharti ahadi hiyo itimizwe.

Wandani wake ambao wameathiriwa na mabadiliko hayo ni Seneta John Kinyua (Laikipia), wabunge Moses Kuria, (Gatundu Kusini), Kimani Ichung'wa (Kikuyu), Alice Wahome (Kandara), Cecily Mbarire (mbunge maalum) na Catherine Waruguru (Laikipia).

Lakini licha ya mageuzi hayo, wananchi, viongozi wa makundi ya vijana, wanaharakati wa kisiasa kati ya wadau wengine Mlimani wanashikilia kuwa kwa "kumwadhibu" Dkt Ruto, Rais Kenyatta anasahau kwamba anaendelea kumpa umaarufu mkubwa miongoni mwa viongozi na wafuasi wake.

**MAKANISA**

Kulingana na Bw Eustace Wainaina, ambaye ni kiongozi wa vuguvugu la Mt Kenya Youth for Change (MYC), hali inayomkumba Dkt Ruto ni sawa na waliojipata wakiwa na Rais Kenyatta mnamo 2013, ambapo walikuwa wakikabiliwa na mashtaka ya uhalifu katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Bw Wainaina anasema kuwa watu wengi katika Mlima Kenya na Bonde la Ufa walijitokeza kuwapigia kura wawili hao kuwaonyesha uungwaji mkono na kama uasi dhidi ya ICC.

"Rais Kenyatta anasahau kwamba kwa kuendelea kumwelekeza Dkt Ruto mijeledi ya kisiasa, anamjenga, sawa na walivyojengwa na aliyekuwa Kiongozi wa ICC, Luis Moreno Ocampo. Wakenya wengi waliwapigia kura kama huruma kutokana na mashtaka yaliyowakabili," akasema.

Wananchi wengi wanasema kuwa Dkt Ruto amefanikiwa kujijengea ufuasi, hasa kwenye makanisa.

Wengi pia wanasema amekuwa akitoa misaada yake ya chakula kupitia Wakfu wa Samoei Ruto (SRF) kwa kuwatumia viongozi wa makanisa na kijamii.

"Dkt Ruto amebuni mbinu ambapo anawasiliana moja kwa moja na wananchi kwa kuwatumia viongozi wa wananchi mashinani. Ni hatua ambayo imeimarisha sana mwingiliano wake na wakazi mashinani," asema Mzee Mwangi Gichuhi, ambaye ni kiongozi wa kanisa moja katika eneo la Mathira, Kaunti ya Nyeri.

Kabla ya "adhabu" dhidi ya wandani wake kuanza, Dkt Ruto alikuwa akiandamana na wabunge hao, huku wakiwakumbusha wenyeji kutosahamu "alivyomsaidia" Rais Kenyatta kutwaa urais 2013 na 2017.

Baadhi ya wananchi ambao hawakutaka kutajwa walisema kuwa isingekuwa ni mchango wa Dkt Ruto, Rais Kenyatta hangeibuka mshindi kwenye chaguzi hizo mbili.

"Ufasaha wa Dkt Ruto ulikuwa nguzo kuu sana kwa kampeni za Jubilee. Ana uwezo mkubwa kujieleza ikilinganishwa na Rais Kenyatta. Kwa kiwango kikubwa, semi zake ndizo ziliwavutia wananchi wengi," asema Bw Moses Nderitu, ambaye ni kiongozi wa kundi moja la kijamii katika Kaunti ya Nyandarua.

Kando na hayo, wanasema kuwa wengi walitazama mchango muhimu ambao alitoa kwenye ushindi wa Rais Kenyatta.

"Rais Kenyatta na Dkt Ruto wamekuwa wakionekana kama pacha kisiasa, kutokana na msimbo wa 'UhuRuto.' Licha ya tofauti zilizopo kati yao, jamii za Mlima Kenya—Agikuyu, Aembu na Ameru, bado zinamwona Ruto kama mmoja wao kutokana na uhusiano wake mrefu na Rais Kenyatta," asema Bw Wycliffe Muga, ambaye ni mchanganuzi wa siasa.

# Leopards kuwa na uwanja wao rasmi



KIONGOZI wa ANC Musalia Mudavadi (pili kulia) akiwasilisha hundi mwigo ya Sh633,000 kwa Mwenyekiti wa AFC Leopards Dan Shikanda (tatu kulia) ili kuisaidia AFC kuanza kutayarisha haki miliki ya shamba lao eneo la Kasarani, Nairobi. *Picha/Hisani*

NA JOHN ASHIHUNDU

Sasa ni rasmi kuwa AFC Leopards itakuwa klabu ya kwanza nchini Kenya kumiliki uwanja wa michezo.

Hii ni baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais, Musalia Mudavadi aliye mlezi wa klabu hiyo kuikabidhi Ingwe Sh633,000 kugharamia usajili wa ardhi iliyopewa na Hayati Mzee Daniel Arap Moi mnamo 1992.

Kulingana na stakabadhi, ardhi hiyo ya ekari 20 inakaribiana na uwanja wa Kimataifa wa MISC, Kasarani.

Akiikabidhi Ingwe shamba hilo kama shukrani kwa kuvuma katika soka nyakati hizo, kadhalika Marehemu Moi aliipatia Gor Mahia kipande kama hicho.

Leopards ilikuwa imeshinda ubingwa wa CECAFA milele, wakati ambapo Gor Mahia walikuwa wametwaa ubingwa wa Mandela Cup.

Akitoa pesa za kugharamia usajili wa adhi ya Ingwe, Mudavadi alisema angependa kuiona Leopards ikiwa na 'boma lake' la kudumu.

"AFC Leopards ni timu iliyo na wafuasi wengi, na pia mfano mzuri kwa vijana wengi wanaotaka kupiga hatua katika usakataji soka. Tungependa kuchangia katika mradhi huu muhimu, wakati tunaendelea kuisaidia wachezaji kifedha wakati huu mgumu wa janga la corona," alisema kiongozi huyo wa chama cha Amani National Congress Party (ANC).

Aliyekuwa mwenyekiti wa klabu hiyo, Alfred Sambu ambaye ni Mbunge wa Webuye West alisema kusimamia soka barani Afrika, hasa nchini Kenya ni mzigo mkubwa hasa timu inapokosa ufadhili.

"Nilipokuwa mwenyekiti AFC Leopards, Mudavadi alikuwa mlezi na aliniunga mkono kikamilifu. Wakati huo wachezaji wetu wengi walikuwa wafanyakazi katika mashirika ya umma, kinyume na siku hizo ambazo maisha ni magumu kutokana na ukosefu wa ajira kwa vijana wewngi wanaotaka kusakata soka," alisema Sambu ambaye aliiongoza Leopards kwa viupindi viwili tofauti.

Akimpongeza Mudavadi kwa usaidizi wake wa kifedha, mwenyekiti wa Leopards, Dan Shikanda alisema atahakikisha Ingwe imepata cheti cha haki miliki ya ardhi hiyo haraka iwezekanavyo.

# Nyota wa Gor tayari kutandaza gozi baada ya kupona

NA CECIL ODONGO

BEKI wa Gor Mahia Philemon 'Mbish' Otieno amesema kwamba sasa yupo fiti kabisa kurejea uwanjani baada ya kuwa mkekani kwa muda wa miezi tisa. Otieno, ambaye alirefusha kandarasi yake na Gor Mahia kwa miaka miwili Januari, alikuwa na jeraha la goti liliilomweka nje kwa karibu msimu mzima. "Umekuwa mwendo mrefu, lakini hatimaye nafurahi kuwa fiti tena kusakatia timu yangu. Madaktari wangu na wale wa timu wameniruhusu nirejee uwanjani baada ya kukamilisha matibabu na kupona. "Ningependa kuwashukuru mashabiki wa K'Ogalo na benchi ya kiufundi wakiongozwa na kocha Steven Polack kwa kunivumilia muda huo wote na hata kurefusha kandarasi yangu," akasema Philemon kwenye mahojiano na ***Taifa Leo***.

Aidha, mwanadimba huyo aliahidi kupigania nafasi yake ambayo imekuwa ikihimiliwa na Geoffrey Ochieng' na Michael Apudo wakati amekuwa mkekani. Otieno alikuwa akijitokeza mara kwa mara kuhudhuria mazoezi na wachezaji wengine ugani Camp Toyoyo kabla ya ligi kusitishwa Machi kutokana na janga la corona. Alipata jeraha akisakatia timu ya taifa Harambee Stars kwenye mchuano wa kufuzu kushiriki soka ya CHAN dhidi ya Tanzania Julai mwaka jana. Kenya iliibanduliwa nje na Tanzania kwenye kipute hicho mwaka jana. Shirikisho la Soka Nchini (FKF) na klabu ya Gor zilikataa kugharimia matibabu yake. Familia yake ilimtibu kwa kima cha Sh350,000 hadi akapona jeraha hilo.



BEKI wa Gor Mahia Philemon Otieno audhibiti mpira katika mechi yao dhidi ya KCB FC katika uga wa Kenyatta, Machakos mwaka jana. Mbish amesema kwamba sasa yupo fiti kabisa kurejea uwanjani baada ya kuwa mkekani kwa muda wa miezi tisa. *Picha/Maktaba*

## Kwa Ufupi

TURKANA

### Majembe yalima Lokitang FC 3-1

**MAJEMBE** FC iliikung'uta Lokitang' FC 3-1 katika mechi ya kupimana nguvu uwanjani Sunset, Ijumaa. Bao la kwanza la Majembe lilipachikwa wavuni dakika ya 18 kupitia kwa John Tioko. Simon Lomong'in lilisukumwa wavuni dakika ya 68. Bao la tatu lilifungwa dakika ya 80 kupitia kwa Enock Lomisi. Lokitang' ilipata bao la kufutia machozi dakika ya 64 kupitia kwa mshambuliaji matata Julius Lomisi baada ya kuandaliwa pasi safi na Joshua Ekwom.

BAMBURI

### Pendua yageuza Majaoni kitoweo

**PENDUA** Rangers FC iliikwaruza Majaoni Stars mabao 5-0 katika mchuano wa kujipima nguvu uwanjani Majaoni Wanders, Ijumaa. Rangers ilitawala mchuano huu. Mabao ya Rangers yalifungwa na Emmanuel Katana, John Kalinga na Abdallah Ibrahim katika kipindi cha kwanza na Erick Wamalwa na Mohammed Kassim katika kipindi cha mwisho. Wachezaji wa Majaoni Stars walionekana kutokuwa katika utimamu wao hivyo kushindwa kuhimili kasi ya wapinzani wao.

*Na Charles Ongadi*

KATHIANI

### Ting'ang'a, Katisaa ni vikong'oto kweli!

**KLABU** ya Ting'ang'a ya kocha Kioko Sing'ali iliilemea Soweto Wazee FC 3-1 kwenye mchuano mkali wa kupimana nguvu katika Shule ya Msingi ya Kathese, juzi. Ting'ang'a iliona lango ya kwanza dakika ya 23 kupitia kombora la Mbuvu Kitu. Mvamizi Munyao Musyoka alimimina wavuni mabao mengine dakika ya 32 na 43. Soweto Wazee ilipata bao la kufutia machozi kupitia jitihada za Mutuku Maingi katika kipindi cha lala-salama. Kwingineko, Katisaa ilibomoa Five Hills 3-0 uwanjani Manza.

*Na Cornelius Mutisya*

THIKA

### Ndarugu Stars tayari kushiriki ligi

**NDARUGU** Stars FC inajiandaa kucheza mechi za ligi ndogo ya kaunti ya Thika msimu ujao. Kocha James Kimani amesema kuwa mambo yakirejea kawaida watajikusanya pamoja kama timu na kuanza mazoezi ya pamoja. Timu hiyo imekuwa ikishiriki mechi za kuwania mataji na za kirafiki, lakini wakati huu imeamua kupiga hatua zaidi. Hata hivyo, Kimani amewaomba wahisani na mashabiki wasilegeza kamba kwa kuwasahau kwani wanahitaji msaada wa kifedha.

*Na Lawrence Ongaro*

# Kocha asalia bubu kuhusu mchujo ambao unanukia Bandari FC

NA ABDULRAHMAN SHERIFF

KOCHA Ken Odhiambo ***(pichani)*** alikataa kuzungumza lolote juu ya uvumi unaoenea kuwa timu yake ya Bandari FC inapanga kuchuja wachezaji katika kikosi cha zaidi ya 30 imeajiri hadi 25. Habari zimeenea mjini Mombasa zikidai kuwa viongozi wa Bandari wanafanya mpango huo.

Viongozi hao hawakupatikana kuthibitisha kama kuna ukweli wowote wa uvumi huo. Afisa Mkuu wa Bandari FC, Edward Oduor pia hakupokea simu alizopigiwa. Odhiambo alisema hana la kusema hadi watakapokutana mazoezini serikali itakapoondoa marufuku dhidi ya mikusanyiko ya watu.



"Wakati huu unafahamu kuwa hatuwezi kufanya lolote sababu tuko nyumbani kujikinga kwa virusi vya corona. Tukiwa uwanjani, tutatambua mipango itakayokuwa imefanywa," akasema Odhiambo.

Mashabiki wa kandanda wa jimbo la Pwani wana hamu ya kujua wachezaji watakaotemwa na wale watakaobakia timuni.

# Nileteeni Mmexico aone, ahaha Zarika

Na CHRIS ADUNGO

FATUMA Zarika angali na kiu ya kuchapana makonde na bingwa wa sasa wa taji la WBC, Yamileth 'Yeimi' Mercado wa Mexico. Ni matarajio ya Zarika kwamba Yeimi ataridhia kurejea ulingoni kunyanyuana naye kwa mara nyingine licha ya mapromota wa malkia huyo wa dunia kusita kuidhinisha mpangilio huo ambao mchakato wake ulianza Januari 2020.

Zarika alimzidi Yeimi maarifa kwa wingi wa alama walipochapana kwa mara ya kwanza mnamo Septemba 8, 2018 jijini Nairobi. Marudiano yaliyoandaliwa mjini Chihuahua, Mexico mnamo Novemba 16, 2019 yalishuhudia Yeimi akilipiza kisasi na kumdengua Zarika kirahisi kwa alama 99-91, 98-92 na 99-91. Hadi walipomenyana, Zarika alikuwa mshikilizi wa taji la WBC kwa kipindi cha miaka minne na akalitetea mara tatu kwa mafanikio tangu 2016.

Japo Zarika alitumainia kwamba WBC wangalimratibu kuvaana tena na Yeimi, bondia huyo wa Mexico amepangiwa sasa kupimana ubabe na Catherine Phiri wa Zambia katika juhudi za kutetea ubingwa wa taji hilo.

Mchapano kati ya Yeimi na Phiri ulitarajiwa kufanyika nchini Mexico mnamo Machi 2020. Hata hivyo, uliahirishwa hadi Septemba kutokana na kanuni mpya zinazodhibiti usafiri miongoni mwa mataifa mengi baada ya mlipuko wa virusi vya homa kali ya corona.

Japo anakiri kwamba marejeo yake ulingoni hayatakuwa rahisi, Zarika ameshikilia kwamba atapania kukabiliana vilivyo na ushindani mkali kutoka kwa Yeimi iwapo ombi lake la kuchapana naye litazingatiwa na kuidhinishwa.

Hadi serikali ya Nchi za Milki za Kiarabu (UAE) ilipoamrisha kufungwa kwa maeneo yote ya umma kutokana na janga la corona mnamo Machi 15, 2020, Zarika alikuwa akifanya mazoezi katika ukumbi wa Round 10 Gymnasium jijini Dubai.

Amefichua pia azma ya kupunguza uzani na kuanza kushiriki ndondi za flyweight ili kuzidisha matumaini ya kutia kibindoni mataji mengine zaidi katika ulingo wa ndondi kabla ya kustaafu. Anashikilia kuwa atapania kushiriki mapigano ya kitaifa na ya kimaeneo yanayofikia raundi nane pekee kabla ya kujitosa ulingoni kunyanyuana na wanamasumbwi maarufu zaidi duniani hapo baadaye.

Nation Media Group "Digital Copy"

TAIFA JUMAPILI

# spoti

## MATUMAINI YA INGWE KUMILIKI UWANJA ENEO LA KASARANI UK15



Fowadi wa Real Madrid, Gareth Bale asherehekea baada ya kufungia timu yake dhidi ya Girona FC uwanjani Montilivi mjini Girona hapo zamani. *Picha/Maktaba*

# SIRUDI 'MISRI'

**LONDON, UINGEREZA**

NYOTA Gareth Bale hataki kurejea tena kusakata soka ya Ligi Kuu ya Uingereza (EPL) na dalili zote zinaashiria kwamba ataangika daluga zake ulingoni akivalia jezi za Real Madrid. Haya ni kwa mujibu wa wakala wake, Jonathan Barnett.

Bale, 30, amekuwa akihusishwa na uwezekano mkubwa wa kurejea Tottenham Hotspur au kuingia katika sajili rasmi ya Newcastle United mwishoni mwa msimu huu baada ya uhusiano wake na kocha Zinedine Zidane kuvurugika uwanjani Santiago Bernabeu.

Fowadi huyo mzawa wa Wales aliondoka Tottenham mnamo Septemba 2013 kwa kima cha Sh11 bilioni na amewashindia Real mataji manne ya Klabu Bingwa Ulaya (UEFA), moja la La Liga, moja la Copa del Rey, matatu ya Kombe la Dunia miongoni mwa klabu, matatu ya Uefa Super Cup na moja la Spanish Super Cup.

Bale mwenye umri wa miaka 30 alitarajiwa kuingia katika sajili rasmi ya Jiangsu Suning ya China kwa mkataba wa miaka mitatu mwanzoni mwa msimu huu huku akipokezwa mshahara wa hadi kufikia kima cha Sh130 milioni kwa wiki.

Hata hivyo, Real walizuia uhamisho wake katika dakika za mwisho kwa sababu walitaka Suning walipie ada yote ya kumsajili na pia walikuwa bado wakimhitaji baada ya winga Marco Asensio kupata jeraha.

Inter Miami ya kocha David Beckham nchini Amerika pia iko tayari kuweka mezani Sh7 bilioni kwa minajili ya huduma za Bale.

"Anafurahia maisha yake jijini Madrid. Sioni sababu itakayomfanya kutostaafu akiwa mchezaji wa Real," akatanguliza Barnett.

"Iwapo ni pesa, anazo. Aidha, ameshinda takriban mataji yote ya haiba kubwa katika ulingo wa soka isipokuwa Kombe la Dunia miongoni mwa mataifa. Bahati mbaya yeye ni mchezaji wa Wales na ndoto ya kuongoza taifa hilo kutwaa ubingwa wa dunia huenda isitimie," akasema Barnett.

Kupungua kwa mapato ya Real msimu huu kutokana na janga la corona kunatarajiwa pia kuwaweka miamba hao wa soka ya Uhispania katika ulazima wa kuwatia baadhi ya wanasoka wao mnadani mwishoni mwa muhula huu.

Miongoni mwao ni kiungo mvamizi wa Colombia, James Rodriguez aliyewahi pia kuchezea Bayern Munich kwa mkopo.

**BERLIN, UJERUMANI**

## Bremen tayari kuroroma Bundesliga

ITAKUWA ni mguu niponye kwa Werder Bremen na VfL Wolfsburg katika mechi ya raundi ya 30 ya Ligi Kuu ya Ujerumani (Bundesliga) itakayowakutanisha leo uwanjani Weser.

Huku Bremen wakipigania fursa ya kuponea chupuchupu na kusalia kwenye kampeni za Bundesliga muhula ujao, Wolfsburg wanalenga kuwapiku Hoffenheim na kuepuka hatari ya kupitwa na Freiburg, Hertha Berlin na Schalke katika vita vya kufuzu kwa gozi la Europa League msimu ujao.

Matumaini ya Bremen kuponea shoka la kuwateremsha daraja mwishoni mwa muhula huu yalididimizwa zaidi Jumatano iliyopita baada ya kupokezwa kichapo cha 3-0 na Eintracht Frankfurt waliokuwa jana wageni wa Hertha.

Matokeo hayo ya Bremen yaliwaning'iniza padogo zaidi mkiani mwa jedwali kwa alama 25 baada ya mechi 29 na kwa sasa wao na limbukeni Paderborn ndio wanaotazamiwa kushuka daraja zikisalia mechi tano pekee kwa kampeni za msimu huu kutamatika rasmi.

Kwa upande wao, Wolfsburg wanapigania nafasi ya kumaliza miongoni mwa vikosi sita-bora kileleni mwa jedwali ili kunogesha soka ya bara Ulaya kwa msimu wa pili mfululizo. Watajibwaga ugani wakitawaliwa na kiu ya kujinyanyua baada ya chombo chao kuzamishwa kwa 2-1 na Eintracht Frankfurt wikendi iliyopita.

Kwingineko, mshambuliaji wa Southampton, Shane Long, 33, ametia saini mkataba mpya wa miaka miwili katika makubaliano ambayo kwa sasa yatamdumisha uwanjani St Mary's hadi mwishoni mwa msimu wa 2021-22.

Nyota huyo mzawa wa Jamhuri ya Ireland alisajiliwa na Southampton mnamo 2014 baada ya kuagana na Hull City.

Long anajivunia kufungia Southampton mabao 35 na mchuano wake wa 200 ndani ya jezi za kikosi hicho ulikuwa ule uliowashuhudia wakipokea kichapo cha 1-0 kutoka kwa Newcastle United mnamo Machi 7, 2020.

Haya yanajiri siku chache baada ya kocha Ralph Hasenhuttl, 52, kutia saini mkataba mpya wa miaka minne na kikosi hicho hadi 2024.

Ukiwa na suala lolote ungetaka kuwasilisha kwetu, tuma sms bila malipo kwa 20684 ukianza na neno 'Taifa'

Taifa Jumapili

6 161105 100164

Hutayarishwa katika Nation Centre, Kimathi Street, na kuchapishwa Mombasa Road, Nairobi, na kampuni ya Nation Media Group, S.L.P. 49010, GPO Nairobi 00100, Simu: 3288000, 0719038000, Fax: 2213946. Ime orodheshwa katika Posta Kuu kama Gazeti.

Nation Media Group "Digital Copy"